


USHUHUDA BAHARINI

 Kabla hatujainamisha vichwa vyetu kwa maombi, ningetaka kusoma sehemu ya Neno la Mungu. Daima napenda kusoma Neno Lake; kwa sababu maneno yangu yatashindwa, ni ya mwanadamu, bali Neno Lake haliwezi kushindwa. Nanyi mnaolifuatilia somo, na kadhalika, hebu tusome kutoka Mathayo sura ya 14, usiku wa leo, tukianza na aya ya 22.

Mara Yesu anawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake.

Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi; maana upepo ulikuw wa mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaenda, akienda kwa miguu juu ya bahari.

Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.

Mara Yesu akanena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiope.

² Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Wakati vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu, je! kuna haja kwenye jengo hili, usiku huu, ambayo ungetaka kumjulisha Mungu, kwa kuinua mikono yako, na ukumbukwe katika maombi? Bwana na awaangalie, aturehemu.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa katika Uwepo Wako, kwa njia na Jina la Bwana Yesu. Tukijua, kwa matumaini yaliyobarikiwa, ya kwamba Yeye alituahidi, kama “tungeomba lo lote” katika Jina Lake, ya kwamba Wewe ungetujalia jambo hilo. Tuna shukurani sana kwa ajili ya jambo hili. Maneno hayawezi kueleza jinsi tunavyojisikia juu ya jambo hilo, tukiwa na kuwa na hakika tuliyo nayo, ya kwamba Wewe unatusikiliza sasa hivi.

⁴ Umeona mikono hiyo, Bwana. Unajua walikuwa na haja gani. Wewe ni Mungu ajuaye yote, mwenye nguvu zote, asiye na mwisho, nasi tunajua ya kwamba Wewe unajua mioyo ya watu. Ulijua mawazo yetu. Hata kabla hatujaumbwa, ulijua kila wazo ambalo tungepata kuwa nalo, kwa maana Wewe huna mwisho.

⁵ Nasi tunaomba, Bwana, kwenye saa hii, kwa kuwa shauku zetu ni kukufikia Wewe, angalia kutoka Mbinguni, Bwana, na utie maombi yetu katika moyo Wako Mwenyewe, Bwana na utujibu kulingana na utajiri Wako huko Utukufuni. Tupe shauku za moyo wetu, tukiamini ya kwamba hayo ni mapenzi Yako ya Kiungu. Nasi twajua kwamba ni mapenzi yako mema kufanya mapenzi Yako.

⁶ Tupe kumwagwa kwingi kwa Uwepo Wako, usiku wa leo, tena Bwana. Waponye wagonjwa. Waokoe waliopotea, wafufue hao waliokufa katika dhambi na makosa, na uwalete kwenye Maisha mapya, usiku wa leo. Naomba tumwone Yesu. Tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

⁷ Mwaweza kuketi. Tunasikitika ya kwamba hatuwezi kuwapatia watu nafasi, kwa ajili ya nafasi ya kuketi. Bali tangu usiku wa kwanza, wao wanasema imewalazimu kuwaondoa umati wa watu wengi sana, kwa hiyo tunasikitika kwa ajili ya jambo hilo. Wala naye Ndugu Grant hakuweza tu kumaliza kabisa kujenga chumba kingine, wala ku. . . Naamini ni kwenye upande wa kushoto anakotaka kuupanua ukuta huu. Ndugu huyu mpendwa sasa, mpendwa sana aliniomba kama ningeweza kulifanya jambo hili kuwa jambo la kila mwaka, kurudi tena Dallas, kwenye kanisa lake. Mwaliko mkubwa namna hiyo, katika saa hii, wakati milango inafungwa haraka sana, halafu mtu huyu anataka nirudi na kulifanya jambo la kila mwaka, kazi ya kudumu. Nathamini jambo hilo.

⁸ Nilikuwa na wakati wa ushirika pamoja nao asubuhi ya leo, pamoja na Ndugu Gordon Lindsay na wengi wao. Ndugu Pearry Green, ambaye ndiye mdhamini wa mikutano ijayo kule Beaumont, anayeketi nyuma yangu hapa usiku wa leo. Na wengi, marafiki zetu, Ndugu Don pamoja na mkewe. Tuna furaha sana kuwa nao hapa. Bwana awabariki.

⁹ Sasa, usiku wa leo, kunini tu. . . Nimekuwa nikijaribu kuzifanya Jumbe zangu rahisi sana ziwezavyo kuwa, ili kwamba hata mtoto angeweza kuzipata.

¹⁰ Kesho alasiri ni ibada ya uinjilisti, nami ningependa nyote mhudhurie.

¹¹ Sasa kama una ibada kanisani kwako, mbona, wewe— wewe kaa mahali ulipo—mahali ulipowekwa. Hatutaki mtu ye yote aache kanisa lake, ku-. . . Halafu basi kama wewe ni mgonjwa na unataka kuja kuombewa, na kanisa lako lina ibada kesho alasiri, nena na mchungaji wako juu ya jambo hilo, ili kwamba asifikirie vibaya, wajua. Hebu ajue ya kwamba tuko hapa kushirikiana, ku—kuusaidia Mwili wote wa Yesu Kristo unaoishi hapa Dallas na vitongoji vyake.

¹² Kwa hiyo, kesho alasiri, nafikiri, kwenye saa nane na nusu, nitahubiri Ujumbe wa kiinjilisti. Kisha tutawaombea

wagonjwa wote, tuchukue kadi zote za maombi na mambo ambayo yameachwa juma nzima na kuombea yote kesho.

¹³ Sasa somo langu usiku wa leo ni zaidi kama mchezo mdogo wa kuigiza, kwa muda mfupi tu. Nami nitajaribu kuwaingiza wengi sana niwezao usiku wa leo, katika kuwaombea wagonjwa. Fungu langu la maneno ni, “msiogope, ni Mimi,” Yesu akinena. Somo langu ni: *Ushuhuda Baharini*

¹⁴ Hapana shaka ilikuwa kwenye machweo, jua lazima lilikuwa likitua wakati jambo hili lilipotukia, na sasa lazima ilikuwa ni siku yenye joto kama ilivyo hapa.

¹⁵ Kiyoyozi hakifanyi kazi, nao wanakitengeneza. Hiyo ndiyo sababu nilibadilisha somo langu kutoka kule, lile nililokuwa nizungumzie, ili kwamba nipate kuliharakisha, ili kwamba msiketi kwenye joto kama hili.

¹⁶ Huyu mvuvi mkuu, baada ya kuona kile alichokuwa nacho siku nzima, alikuwa akimwangukia Yesu katika huduma Yake kuu.

¹⁷ Ningalipenda sana kuishi katika siku hiyo, kumfuata Yeye. Lakini, mnajua, nina furaha ningali na majaliwa ya kufanya jambo lile lile, kumwangukia akifanya mambo. Na ni jambo kuu zaidi kumwangukia leo kuliko ilivyokuwa wakati huo. Nina imani zaidi katika Yeye sasa, na ninaweza kuwa na imani zaidi sasa kuliko ningaliweza kuwa nayo wakati huo, kwa maana tumekuwa na miaka elfu mbili kuthibitisha ya kwamba Injili ni kweli. Na Baada ya miaka elfu mbili, Yeye yungali hai, akifanya kama vile tu alivyofanya wakati huo, kwa hiyo tuna matumaini makuu zaidi na msingi imara zaidi wa imani sasa kuliko walivyokuwa nao wakati huo.

¹⁸ Kwa sababu, Yeye alikuwa Mtu tu aliyekuwa akizunguka kila mahali na dai fulani ya kwamba—ya kwamba Yeye alitumwa kutoka kwa Mungu na alikuwa Mwana wa Mungu, na ya kwamba Mungu alikuwa anathibitisha Neno Lake la ahadi la siku hiyo, kwa Yeye, nao kwa namna fulani walikuwa na sababu ya kushuku jambo hilo. Wanatheolojia, walishuku! Nanyi mnaona lilikuwa jambo la kuhuzunisha, ilikuwa huzuni kweli, kwa sababu hao wanatheolojia wangaliamini jambo Hilo kama Mungu hakuwa amepofusha macho yao. Biblia ilisema hivyo.

¹⁹ Hivi mnajua Yeye aliahidi angeyapofusha macho yao tena leo, hata wasiweze kuliona? Wao wangukuwa “wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizua, wasiopenda mema; wenye mfano wa utauwa, lakini wangekana nguvu zake.” Kweli ni ahadi tu iliyotimia tena. Nawe ni vigumu kufanya lo lote ila kuwasikitikia tu watu, na macho yao yakipofushwa kwenye siku hii. Pamoja na Maandiko ambayo Mungu ameahidi yangetimia moja kwa moja katika siku hii, katika saa hii, nasi tunaitazama

moja kwa moja na kuichunguza. Halafu watu wanaangalia, na kutikisa vichwa vyao na kuondoka, kusema, “Mimi sioni jambo Hilo.” Ni jambo la kuhuzunisha, bali hata hivyo Maandiko hayana budi kutimizwa. Haina budi kuwa hivyo.

²⁰ Kwa hiyo wanafunzi hawa walikuwa wamechaguliwa na Mungu. Je! umeona, Yesu aliwaambia, “Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” Yeye aliwachagua, nao walikuwa mzao uliochaguliwa na Mungu. Hiyo ndiyo sababu wakati shida zilipotokea, nao watu waliona kama kwamba wamemweka Yesu kwenye kona, kwa swali fulani, hawakuwa na na tashwishi. Wasingeweza kufahamu jambo hilo, bali waliazimia kutojua cho chote ila Yeye. “Wewe tu Ndiwe uliye na Neno la Uzima.” Nao waliazimia kudumu Nalo, kwa maana wao walichaguliwa kwenye utume huo.

²¹ Na ndivyo ilivyo leo, ya kwamba wanaume na wanawake, waliochaguliwa kupata Uzima wa Milele, watafikia Uzima wa Milele. “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Hilo ni Neno Lake, nalo Hilo haliwezi kushindwa. Ni—ni Neno la Mungu.

²² Nasi tunaona hawa wanafunzi sasa, waliokuwa na mkutano mzuri sana siku hiyo, huko nje kwenye uwanja mkubwa karibu na mlima. Naye Yesu alikuwa amewaambia, “Sasa ninyi tangulieni mvuke bahari, mbele yangu Mimi.” Naye alikuwa anapanda mlima, peke yake, akapate kuomba. Na hawa wanafunzi, baada ya kukutana na marafiki, ninaweza tu kuwazia walivyojisikia.

²³ Kwa sababu, kukutana na marafiki, kisha iwabidi kuachana na marafiki; yapata tu wakati umefanya urafiki, kisha inakubidi kusema kwaheri. Na jambo hilo kwa namna fulani daima limenitatiza, kote nchini, na kote ulimwenguni, nimekuwa nikikutana na marafiki kisha ninawaacha, nikijua kuna wengi ambao hutawaona tena mpaka utakapokutana nao kwenye ile Hukumu. Kwa namna fulani ni jambo la kuhuzunisha.

²⁴ Ninaweza kuwazia kile chombo, huku—huku gubeti lake limesukumwa ukingoni. Na lazima ilikuwa ni Simoni Petro, mwenye mikono mikubwa na mabega manene, ambaye aliisukuma ile merikebu na kuilekeza baharini. Nao wote walikuwa wakiwapungia mikono ya kwaheri hao waliokuwa ukingoni. Nao walikuwa wakipiga makele, “Karibuni tena na mumlete Bwana atutembelee. Na mje tuwe na ufufuo mwingine; tumebarikiwa sana leo!” Na marafiki wapya wakiwapungia mikono. Ndipo akapanda juu ya hao wanafunzi wengine, akaketi labda karibu na ndugu yake, Andrea, akachukua makasia.

²⁵ Vyo—vyombo wakati huo viliendeshwa aidha kwa upepo ama makasia waliyovuta. Nao labda wangekuwa wameketi wawili-wawili kwenye chombo, wawili upande mmoja, nao wange- . . . ama wawili kwenye kiti kimoja, hasa, labda makasia sita ama manane. Wao wangeyavuta taratibu, na kwa njia hiyo

wangeweza kuishikilia merikebu kwenye mkuku wake tufani inapovuma. Halafu, pepo zikivuma kawaida, wao wangeweza kutuweka matanga, na kufunga safari.

²⁶ Lazima ilikuwa alasiri yenye joto, tukiangalia Maandiko kabla tu ya tukio hili, na kwa hiyo lazima ilikuwa ni alasiri tulivu sana, yenye jua, na joto. Jua lilikuwa linatua. Nao, walipokuwa wanavuta makasia, kisha wanaachilia na kuwapungia watu mikono ya kwa heri, “Tunatumaini kuwaona tena siku moja,” walipokuwa wanasafiri baharini. Na kutua kwa jua, na ukungu wa jioni, halafu baada ya kitambo kidogo u—usiku ukaingia.

²⁷ Nao lazima walishika mwendo mzuri wa—wa makasia, na hiyo ni kazi ngumu wakati hayo makasia mazito yanapoingia baharini. Na karibu wote walikuwa—walikuwa wavuvi, na watu wenye ngumu mno, waliozoea bahari. Na kwa hiyo walikuwa wakimtarajia Yesu kuingia merikebuni na kuwafuata, baadaye kidogo. Mbona, wao walifika kule, nao hapana budi walivuta matanga kidogo; kwa namna fulani kuifanya merikebu ishike mwendo, kisha unaachilia.

²⁸ Labda kijana Yohana alikuwa wa kwanza kuzungumza, maana yeye ndiye aliyekuwa mdogo sana wa lile kundi. Na lazima ilikuwa ni Yeye aliyesema, “Mimi karibu ninachoka kidogo. Hebu tuachilie matanga kidogo. Tungojee kidogo, si lazima kuharakisha. Yeye bado hajaja, kwa hiyo afadhali tungojee kidogo na tuvute hewa kidogo.”

²⁹ Na alipokuwa ameketi pale akiwa ameinamisha kichwa chake kidogo, hapana shaka alianzisha mkutano wa ushuhuda. Na huo ndio ninaotaka kunena habari zake. Hapana budi ilikuwa ni yeye aliyeinuka kwanza, na kuasema, “Ndugu, hata watu waseme nini, na ni vipi mtu ye yote anavyotaka kutoamini, mimi nina hakika kabisa sasa, baada ya leo, ya kwamba sisi hatumfuati mwigaji. Hatufuati mwingine ila Mungu, kwa maana hakuna mtu ye yote angaliweza kufanya alilofanya leo isipokuwa iwe alikuwa Mungu. Mnajua, alipochukua mikate hiyo akaivunja, na kuwalisha wale elfu tano kule, hilo ndilo jambo la kushangaza sana kwangu. Ingewezekana kuweko na swali mpaka leo hii,” sasa ninarudia tu ushuhuda wake kama ulivyokuwa, “bali hilo limetatuliwa.”

³⁰ Kasema, “Ninaweza kukumbuka miaka kadha iliyopita. Nilikuwa ninaishi kule chini karibu na Yordani. Nami naweza kukumbuka, kama mvulana mdogo, jinsi mama yangu mrembo wa Kiyahudi aliozoea kunichukua, alasiri, na kuniweka pajani mwake na kunipembeza, huko sebuleni, wakati maua mekundu yalipokuwa yakichanua kwenye kingo za Yordani. Naye alikuwa akiangalia upande wa pili wa jangwa, ambako watu wetu waliletwa kupitia jangwa hili. Yeye aliozoea kunisimulia hadithi za Biblia. Moja ya hadithi nzuri sana ninazokumbuka ilikuwa ile ya Mwanamke Mshunami na wakati mvulana wake mdogo

alipokuwa amekufa, na—na nabii akamfufua mvulana huyu mdogo tena katika wafu. Hiyo ilikuwa hadithi ya kufurahisha moyo sana.

³¹ “Bali moja ya hadithi za kufurahisha moyo, na mama alikuwa na mazoea ya kunisimulia, yeye angesema, ‘Sasa, ewe Yohana, wewe ni mvulana mdogo tu; bali nakutaka ukumbuke, wakati unapokua umri, ya kwamba, Yehova mkuu aliwapandisha watu wetu kutoka Misri, nasi tulipitia katika jangwa lile ng’ambo ya ule mto pale. Na wote kwa miaka arobaini, walisafiri kule jangwani, hawana mahali pa kupata nguo, na wala mahali pa kupata chakula. Basi Mungu akashusha mikate kutoka mbinguni, kila usiku, na kuwalisha watu wetu katika jangwani ile, kwa kuwa walikuwa kwenye wajibu wao, wakimfuata Yehova mkuu. Na sasa, siku moja, Yehova atafanyika mwili hapa duniani, katika mfano wa Mtu, ataitwa Aliyetiwa mafuta, Masihi.’

³² “Nami nakumbuka,” yeye angesema, “kama mvulana mdogo, jinsi ambavyo akili zangu za mvulana mdogo zilikuwa zinawazia, kujaribu kuwaza, ‘Hivi Mungu aliwalishaje hao wote, watu milioni mbili na nusu, huko jangwani? Alipataje mikate hiyo yote?’ Nami nilikuwa nikimwuliza mama, ‘Mama, hivi Yeye, hivi Yehova ana—ana majiko makubwa mno huko juu mbinguni, naye angeoka mikate yote, na kukimbia usiku na kuiweka chi—chini, kwa ajili ya hao watu, na zile mbingu kubwa za Yehova zimejaa majiko?’ Yeye angesema, ‘La, mwanangu, wewe ni mtoto mchaga mno kuelewa. Unaona, Yehova ni Muumba. Yeye ahitaji majiko. Yeye hunena tu, nalo Neno Lake linadhihirishwa anapona. Yeye ni Yehova mkuu, Naye alilinena tu. Nao Malaika wakaisambaza ardhini, kwa ajili ya watu.’

³³ “Na leo, nilipomwona Yeye amesimama pale, uliangalia uso wake ulivyoonekana? Hapakuwepo na shaka moyoni Mwake. Nilipanda juu nyuma ya mwamba, nikamwangalia akichukua mkate huo na kuuvunja, na kuwapa nani... Watumishi Wake, sisi, kuigawanya kwa watu. Na basi aliponyosha mkono kuuvunja tena, mkate huo ulikuwa mzima tena. Naye alifanya jambo hilo mara mia nyingi, mpaka kila mtu akashiba, na kulikuwako na vikapu, vilivyojaa, vilivyookotwa. Najua huyo asingekuwa mwingine ila Yehova, kwa maana alitenda kama alivyotenda Yehova. Yehova tu ndiye anayeweza kuumba. Nami najua ya kwamba Mtu huyo si mdanganyifu. Kuna Muumba mmoja tu, naye huyo ni Yehova. Na sasa, katika mambo yote ambayo nimeona, hilo liliniridhisha.

³⁴ “Nataka mjue sasa ya kwamba moyo wangu umejisalimisha kabisa, nami ninaamini kabisa ya kwamba Yeye si nabii tu. Yeye ni nabii, bali ni zaidi ya nabii. Yeye si mwingine ila Yehova Mungu akikaa kati Yetu, kwa maana aliumba mikate, Naye alikuwa na tabia za Yehovah. Si ajabu aliweza kusema, ‘Kama

sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini; bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, nanyi hamwezi kuniamini Mimi, aminini zile kazi, kwa maana zinanishuhudia na kuonyesha kwamba Mimi ni Nani.' Ilionekana kana kwamba watu wangeweza kuona jambo hilo, rahisi."

³⁵ Naye Yohana aliridhika ya kwamba Yeye alikuwa Masihi, Yule ambaye Isaya alisema, "Kwa maana kwa ajili yetu mtoto Mwanamume amezaliwa, naye ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele." Naye Yohana aliridhika kwa sababu ya yale aliyoona. Kijana huyo akitoa ushuhuda wake.

³⁶ Yapata wakati huo, Simoni Petro akasema, "Vema, sasa, hebu kidogo. Kama tutakuwa na mkutano wa ushuhuda, ningetaka kusema kitu. Mnajua, nilishuku sana jambo hilo lote, wakati ndugu yangu Andrea, aliyehudhuria ufufuo wa nabii Yohana, aliyekuwa ameshuhudia ya kwamba Masihi anakuja na angemjulisha Yeye. Nami kidogo nilishuku yale Andrea angeliniambia, kwa maana nimesikia kila namna ya hadithi za Masihi na cho chote kile.

³⁷ "Bali nyinyi ndugu wote mnamkumbuka mzee baba yangu. Jina lake lilikuwa Yona. Nanyi mnamkumbuka, jinsi alivyokuwa mwamini mwaminifu. Jinsi ninavyoweza kuwakumbuka mama na baba, na sisi sote, tulipokuwa tunavua samaki kupata riziki yetu, nasi tusingepata samaki; tulihitaji mkate, na jinsi tungeanguka sakafuni na kumwomba Mungu, 'Tupe mawindo leo, Mungu, kusudi tuweze kuuza samaki wetu, na kulipa madeni yetu, tupate chakula.' Na vile tulienda huku baharini, kwenye tufani, na kuthubutu ku—kukabiliana na hizo tufani.

³⁸ "Naye baba, naweza kuona nywele zake zenye mvi zikining'inia mgongoni mwake, siku moja alipokuwa ameketi kwenye kamba za chombo na kuzungumza nami, akisema, 'Simoni, wewe ni kifungua mimba changu. Unajua, daima nimeamini, Simoni, ya kwamba ningemwona Masihi. Watu wetu wamemtazamia tangu Edeni. Nasi tuna hakika kwamba Yeye yuaja, hata ichukue muda mrefu vipi. Hiyo imekuwa miaka elfu nne iliyopita, mnasema. Bali ninaamini ya kwamba Masihi atakuja. Na kila Myahudi ameanini ya kwamba angemwona Masihi katika kizazi chake. Ninatumaini kumwona katika kizazi changu. Bali inaonekana kama, ninazeeka sasa, sina budi kuachana na bahari, ninapata maumivu yangu na uchungu, labda sitamwona katika wakati wangu. Lakini labda wewe utamwona, mwanangu.

³⁹ "Nami nataka kukufunza Maandiko. Mwanangu, kabla Masihi hajatokea, mambo ya kila namna yatakuwa yakiendelea, mambo ya uongo wa kila namna, kwa maana Shetani atafanya jambo hilo, kuharibu ushawishi wa Masihi wa kweli atakapokuja." Daima imekuwa namna hiyo; ingali hivyo.

40 Halafu tunaona, yeye alisema, “Nakumbuka alinikumbatia kwa mikono yake, kasema, ‘Mwanangu, kuna njia moja tu utakayoweza kumtambua Masihi huyu. Sasa tumekuwa na mamia ya miaka bila nabii ye yote. Malaki alikuwa ndiye nabii wetu wa mwisho. Hiyo imekuwa miaka mia nne iliyopita, hatujakuwa na nabii. Lakini kumbuka, Musa alitwambia, katika Maandiko, ya kwamba, Masihi ajapo, angekuwa nabii, atakapotokea. Sisi Wayahudi tumefundishwa kumwamini nabii. Na safari ya Masihi duniani ni Neno la Mungu lililonenwa, ambalo Yeye ametuahidi. Nalo Neno daima huja kwa nabii, naye nabii hulithibitisha Neno hilo. Usisahau jambo hilo kamwe, mwanangu! Huenda kukazuka mambo mengi, huenda kukatokea shauku nyingi na—na mambo makuu. Lakini kumbuka, Masihi atakuwa nabii, maana tunajua ya kwamba Mungu kamwe habadilishi njia Yake, Naye alisema ya kwamba Masihi angekuwa nabii. Kwa hiyo, kumbuka mwanangu, manabii ni wale walio na Neno la Bwana. Na Masihi ajapo, Yeye atakuwa nabii.’

41 “Ningali tu naweza kuuhihi mkono wake,” akasema Simoni, “aliponikumbatia. Naye Andrea alikuwa amesimama pale akitengeneza wavu, wakati huo. Unakumbuka hilo, Andrea?”

“Naam, Simoni, na—nakumbuka jambo hilo.”

42 “Naye Andrea akijaribu kuniambia ya kwamba huyu Yohana alikuwa nabii. Nilikuwa na mambo mengine ya kufanya, ilinibidi kuuza samaki na vikorokoro. Kwa hiyo baba ameaga dunia miaka mingi, lakini daima niliweka jambo hilo moyoni; baba alisema, ‘Masihi huyu atakuwa nabii aliyetambulishwa Kimaandiko, na msisahau hilo, kwa maana ni Neno lililonenwa la Mungu. Na hilo Neno daima sikuzote huwajilia manabii; ambao walilitambulisha, ama kudhihirisha yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo.’”

43 Na sasa Simoni, “Siku moja,” kasema, yeye alisema, “unajua, Andrea aliniomba nihudhurie mkutano. Nami nikashuka nikaenda kule mkutanoni ambako Jamaa huyu, Yesu, alikuwa. Nami nilikuwa nimesikia kila namna ya uvumi. Kulikuwako na Yesu fulani aliyeinuka, kabla Yake, aliyeahidi kuwa kitu fulani kikubwa, akaondoka na watu mia nne nao wote wakaangamia, na kadhalika. Nilifikiri ilikuwa ni mwingine tu wa aina hiyo, mwenye namna fulani ya shauku kubwa za ufufuo fulani, ama madhehebu fulani makubwa waliyokuwa wataunda. Lakini siku moja nikafikiri ningeambatana na Andrea hapa, ndugu yangu.”

44 Nami naweza kuwazia, yapata wakati huo, kile chombo kikaanza kutikisika. Mtu fulani akaanza kupiga makelele, na kusema, “Ketini chini! Msifanye chombo kiende mrama. Ngojeni kidogo. Tulieni.”

45 Naye akasema, “Mwajua, niliposhuka nikaenda kule nikasimama mbele Yake, mara ya kwanza, Yeye alinitazama moja kwa moja machoni na kuniambia jina langu ni nani. Hakuwa ameniona hapo kabla. Si kwamba tu alinjua, bali alimjua yule baba yangu mzee mcha Mungu, aliyekuwa amenihekimisha katika Maandiko. Nami nilijua ya kwamba Huyu alikuwa ni Masihi. Hilo lilitosha kwangu mimi, papo hapo. Hilo lilitosha. Hilo lililifanya halisi, kwangu.”

46 Lazima ilikuwa ni Filipo aliyesema, “Hivi naweza kusema Neno hapa?” Sasa akasema, “Ndugu Nathanaeli, usiache hili lisikuumize; kwa sababu, unajua tulisoma yale magombo kwa miaka kadha wa kadha, kile Masihi angekuwa. Bali nilipomwona akifanya jambo hilo, nilikimbia nikamleta rafiki yangu hapa, Nathanaeli. Basi alipokuja huku . . .”

Nathanaeli akasema, “Hebu nilisimulie. Hebu nilisimulie.”

47 Loo, unajua, kuna jambo fulani wakati Yesu amekufanyia jambo fulani, ni vigumu kwako—kwako kutulia, huna budi kulisimulia, wewe mwenyewe. Sivyoy? Kama ni jambo fulani halisi, huna budi kulisema. Wakati aliponijaza na Roho Mtakatifu, ninataka kusimulia jambo hilo. Nataka mtu fulani ajue jambo hilo. Si ati mwingine alisimulie; nataka kulinena, mimi mwenyewe.

48 Nami nawaza tu, Nathanaeli alichajawa na shauku na akasema, “Mnajua, ningetaka kusema jambo hili. Nilikuwa nikikushuku kidogo, Filipo, uliponiambia. Nilikuuliza, ‘Laweza neno jema kutoka Nazareti?’ Nawe ukanipa jibu zuri kabisa ambalo mtu ye yote aliwahi kupata, ‘Njoo uone.’” Hilo lafaa sana mpaka leo hii. Hiyo ni kweli. Usikae nyumbani na kutoa makosa. Njoo, ujionee mwenyewe, unaona. “Kaseam ‘Laweza neno jema kutoka Nazareti?’ Kasema, ‘Njoo ujionee mwenyewe.’ Nawe unajua uliyokuwa umeniambia.

49 “Namini wakati nilipokwenda mbele Zake, Naye akaniambia ya kwamba nilikuwa ‘Mwe—Mwebrania, Mwisraeli, na nilikuwa mtu mwaminifu,’ nilijua jambo hilo.

50 “Lakini nilishangaa, ‘Ingewezekanaje?’ Yeye alionekana kama mtu wa kawaida. Nilikuwa nikimtaazama Masihi ashuke kwenye ukumbi wa dhahabu kutoka Mbinguni, moja kwa moja hata kwa kiongozi wa madhehebu hapa, aende Yerusalemu, atoke na aseme, ‘Kayafa, nimewasili.’ Bali walitambua, Yeye alitoka Nazareti, kutoka katika jamaa maskini; na kwa kweli amebandikwa jina baya nyuma Yake, kama “mtoto wa haramu.” Huyu hapa amesimama, amevalia nguo za kawaida, si kama kuhani ama mtu fulani; mtu wa kawaida tu. Ndipo nikawazia, nilipoenda pale, ‘Huyo anawezaje kuwa ni Masihi? Amevalia joho kuukuu, amelivaa tangu alipokuwa kijana, na hapa amevaa joho lile lile; na nywele Zake zikining’inia mgongoni Mwake. Naye ni kama mtu wa kawaida wa mitaani.’

51 “Naye akaniangalia usoni, na kusema, ‘Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’ Hilo lilitosha. Nilijua, kwa Neno, huyo alikuwa ni Masihi. Huyo alikuwa Ndiye.”

52 Nacho hicho chombo hapana budi kulitikisika, nao mkutano wa ushuhuda ulikuwa unaendelea. Loo, ni wakati mzuri upendezao namna gani waliokuwa nao, huko nje baharini, wakiwa tu na wakati mzuri sana.

53 Andrea akasema, “Mimi ningetaka kusema jambo fulani ambalo kwa namna fulani lilitatiza kwa kitambo kidogo. Mnakumbuka wakati tu—tulipokuwa tunashuka kwenda Yeriko? Yeye alisema, ‘Lazima tukwee; nina haja ya kupitia Samaria.’ Kwa hiyo, akapanda akaenda Samaria na huko katika mji wa Sikari, wakati alitutuma zote kununia vyakula huko mjini.”

54 “Loo, ndiyo, ninakumbuka jambo hilo, sana!” Wote, “En-he, en-he!” Chombo kilikuwa kinatikisika, kila mtu akiwa na ushuhuda wa ajabu baada ya ufufuo kwisha. Kwa hiyo wao walikuwa wanaendeleza mkutano huu wa ushuhuda.

55 Ndipo akasema, “Ndiyo, nanyi mnakumbuka tulichopoka kisirikisiri, na, lo, tulivyoshangaa, tulipomwona Bwana wetu akizungumza na kahaba aliyetiwa alama. ‘A-ha,’ tukawaza, ‘hilo ni jambo baya. Mwone kule anaongea na huyu kijana mwanamke. Naye alitutuma, Naye huyu hapa nje ameketi na mwanamke huyu mwenye sifa mbaya.’ Kumbukeni, tulikuwa tumesimama nyuma tu ya vichaka, nasi tukasikiliza mazungumzo yao.

56 “Nasi tukamsikia akimwambia, ‘Mwanamke, nenda kamwite mumeo, uje hapa naye.’

57 “Nasi tukasema, ‘Vema, huenda tulikosea, labda mwanamke huyu alikuwa ameolewa kihalali.’

58 “Naye mwanamke huyu akamwangalia usoni, na kusema, ‘Bwana, sina mume ye yote.’

59 “Mnakumbuka jinsi mioyo yetu ilivyohuzunika? ‘Masihi wetu mkuu tuliyekuwa na matumaini Kwake, hapa ameshikwa kwenye uongo, amenaswa, maana Yeye alisema, “nenda kamwite mumeo,” naye alikuwa ameshuhudia kwamba hakuwa na mume. Sasa limemrudia.’ Kumbukeni jinsi sisi sote tulivyonekana tumeshangazwa, na pumzi ikatutoka?”

“Naam, ninakumbuka.”

60 “Na tena mnakumbuka maneno yaliyofuata? Akasema, ‘Umesema kweli, kwa sababu umekuwa na watano, naye uliye naye si wako.’ Loo, mnakumbuka ule mkutano wa ushuhuda nyuma ya vichaka? Jamani!” Mnaona, huwezi kumshinda. Yeye ni Mungu. “Loo,” Simoni akasema, “hiyo ilinini tu. . .” Andrea akasema, “Hilo lilitosha kwangu.”

61 Bartholomayo akasema, “Hebu, ningetaka kutoa ushuhuda. Nitoe, ndugu zangu?”

62 “Loo, vema, nadhani unaweza, tuna wakati mwingi sana. Bado hajaja, kwa hiyo tutapiga makafi machache tu. Endelea, Bartolomayo, shuhudia.”

63 “Vema, moja ya mambo makubwa kwangu. Mnakumbuka dada yetu kule chini Yeriko, anayeitwa Rebeka?”

“Naam.”

“Na mumewe ana hoteli kule chini.”

“En-he.”

64 “Na—naye alikuwa mfanyi biashara, na jina lake ni Zakayo.”

“Ndio, ndio, ninamkumbuka vizuri.”

65 “Mnakumbuka, alikuwa—alikuwa mmoja wa dada zetu. Alikuwa amemwamini Bwana, naye alikuwa anahofu sana kwamba Zakayo angeacha yote yapite bila kumkubali Yesu. Na, lo, Zakayo alikuwa rafiki wa pete na kidole wa kuhani pale. Na kwa hiyo alikuwa anaomba ya kwamba jambo fulani lingetendeka kwamba macho yake yangefunguliwa, naye angetambua ya kwamba huyu alikuwa ndiye Bwana, huyu alikuwa ni Neno la Mungu lililothibitishwa, lililofanyika mwili kati yetu. Nasi tulijaribu kumwambia . . . kumwambia kuhusu jinsi Yesu wa Nazareti alivyojua siri za moyo, akionyesha ya kwamba Yeye alikuwa Neno, maana Neno hutambua mawazo ya moyo.

66 “‘Upuuzi,’ akasema, ‘mimi ninamwamini kuhani. Asemayo kuhani yanitosha mimi.’ Kwa sababu alikuwa mfuasi wa ma—mashirika yote mjini, Kiwanis na yo yote yale, mwajua, kwa hiyo kwa namna fulani ni vigumu kwake kuachilia. Kwa hiyo Rebeka alikuwa ametuomba sisi sote tuombe, kuomba. Na kila wakati tungefikia jambo hilo kwamba Yeye ni nabii, yeye angesema, ‘Upuuzi huo! Kuhani anasema, “Yeye ni Beelzebuli. Yeye ni ibilisi. Naye anatenda hayo kwa nguvu za Ibilisi. Na yeye ni mtu tu wa kushirikiana mawazo. Hakuna cha zaidi. Hakuna lo lote.” Kwa hiyo hakuna kitu kama hicho katika siku hizi; hatujakuwa na manabii kwa mamia ya miaka. Basi Jamaa huyo angeweza, bila hata kuwa na kadi la ushirika, Yeye angeweza kuwa nabii? Loo, hawezi kwa vyo vyote kuwa kitu kama hicho!’

67 “Lakini, mwajua, Rebeka, mkewe, aliendelea kushikilia, na kuomba. Na asubuhi moja wakati Yesu alipokuwa anakuja mjini, vema, ndipo tunaona ya kwamba, Rebeka alitwambia ya kwamba Zakayo alikuwa ametoka nje kwenda ba—barabarani, kumwona Yeye. Kwa hiyo hakuamini Yeye alikuwa nabii, kwa hiyo akasema, ‘Nitamwangukia vizuri tu,’ jinsi alivyotushuhudia kule hotelini juzijuzi tulipokuwa tunakula. Kwa hiyo akapanda juu ya mkuyu, na kusema, ‘Wajua nini, nitajificha hapa juu ili asiweze kuniona. Mimi ni mtu mdogo, hata hivyo, mfupi

sana. Nami siwezi kumwona kule chini, katika kundi la watu, kwa hiyo nitapanda tu hapa juu mtini.’ Naye akafikia mahali matawi ma—mawili yanapokutana, akaketi hapo, kwenye matawi haya.”

⁶⁸ Hapo ni mahali pazuri tu pa kuketi na kuchunguza jambo. Hapo ndipo njia mbili zinapokutana, yako na ya Mungu; mawazo yako. Hilo ni jambo zuri, kulichunguza..

⁶⁹ “Kwa hiyo akasema, ‘Mwajua nini, hapana budi Yeye alikuwa ni nabii. Angeweza kuwa hivyo. Ingewezekana ningeweza nikakosea. Kwa hiyo hebu niwaambieni, nitamwangalia vizuri, Naye hatanijua. Kwa hiyo nitachukua majani haya yote na kuyavuta namna *hii*, nijizungushie, nami nitajificha ili kwamba hata hataniona kamwe. Nami nitamwangalia atakapopita. Na kama haonekani ni mtu wa kweli, atanitambua, huku nikiwa nimekaa hapa juu mtini.’ Kwa hiyo akaangalia, naye alikuwa na jani kwa hiyo angeliliinua na kumwona Yeye akipiga kona

⁷⁰ “Basi alipokata kona, akija barabarani, mwajua, akiangalia huko na huko, nao wanafunzi wakisema, ‘Simile. Samahani.’ Huku watu wana watoto wagonjwa na kadhalika. ‘Samahani, Bwana amechoka sana; ibada hiyo kubwa jana usiku. Na, kama muungwana, tafadhali mpisheni. Vema, anashuka Zake mjini, kwa hiyo tafadhali kaeni kando.” Naye Zakayo ameketi hapa juu ya mti, akimwangalia Yeye kule chini.

⁷¹ “Basi Yesu akaja moja kwa moja chini ya ule mti, akasimama, akaangalia juu na kusema, ‘Zakayo, shuka huko mtini. Leo ninakwenda pamoja nawe nyumbani, kula chakula cha mchana.’ Hilo lilitosha. Yeye alijua alikuwa pale juu, na alijua jina lake, kwamba alikuwa ni nani. Hilo lilitosha. Huyu ni Masihi, kwangu mimi. Naam, bwana. Kwa sababu, tunajua Masihi alipaswa kufanya jambo hilo. Bila shaka. Kwa hiyo ilimbidi kwenda nyumbani pamoja Naye, kasema, siku hiyo kula chakula cha mchana. Jinsi huo ulivyokuwa wakati mzuri! Tunakumbuka jambo hilo.”

⁷² Mwajua, lazima ilikuwa wakati kama huo, mkutano wa ushuhuda ulikuwa unaendelea. Mwajua, wanafunzi hawa huko nje baharini, wakishuhudia, lazima ilikuwa kwenye giza kuu la usiku mahali fulani, huko katika nchi za kaskazini kule, ambako hakuna budi Shetani alipanda kilimani na akaangalia chini. Akaangalia kwenye mkutano huo wa ushuhuda, naye akaona kwamba walikuwa wameondoka bila Yeye. Hiyo hapo nafasi yake.

⁷³ Mnaona, nafikiri tamasha hiyo karibu tu imerudi tena, imejirudia. Wao walikuwa, katika furaha za ufufuo, walikuwa wameondoka bila Yeye. Nami naamini ya kwamba hayo ni mengi yaliyotupata leo, kwamba, katika saa hii ya machafuko, na baada ya ufufuo huu mkuu ambao tumeshuhudia. Umezunguka

ulimwengu mzima. Kila taifa limekuwa na kuwashwa kwa mioto ya ufufuo, na inawaka; ibada kubwa za kuponya; watu wakimpokea Roho Mtakatifu kwa maelfu kumi mara elfu kumi. Na katika furaha yake, kama vile wale wanafunzi wakishuhudia yale aliyotenda, “na, loo, tumemwona akifanya jambo *hili*, na tumemwona akifanya jambo *lile*,” ninaamini tumeondoka kama wao, bila Yeye.

⁷⁴ Tumeendea nafasi kubwa mno ili—iliyotolewa na ufufuo. Tumechukua nafasi za kupata pesa nyingi sana, makanisa, kujenga mijengo mikubwa zaidi, mahali pakubwa mno pa mamilioni ya dola, mashule makubwa, miradi ya elimu, na kuyafanya madhehebu yetu yakue. Halafu tunakuwa na mipango yetu ya kikomunisti, kupinga ukomunisti, hayo tu ndiyo tunayoweza kunena juu yake leo. Na jambo la kwanza wajua, Shetani ametuona katika mipango yetu ya kuupinga ukomunisti, kwenye mipango yetu mikubwa ya kimadhehebu, na kwenye “milioni yetu ya zaidi,” na kadhalika, kama waliyo nayo.

⁷⁵ Nasi tumeendelea bila ile mikutano ya zamani ya maombi na kurudishwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, mpaka mioto imefifia. Unaweza kulia, na kujaribu kuwaleta watu madhabahuni, nao wanatembea tu kana kwamba walikuwa karibu wamekufa, wanaogopa sana kuja. Halafu unawaomba wahudumu waje waombe pamoja nao, “Loo, kwa nini akaniomba?” Nao wanashuka wanaenda kule, nawe ni vigumu kuwapata. Nao watasimama pale kwa dakika chache tu, wakuangalie, kisha warudi wakaketi vitini mwao. Kwangu mimi, moto umezima! Jambo fulani limetukia. [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.] Sikilizeni! Tunachohitaji ni ufufuo, ambapo wenye dhambi, wakimwangualia Kristo, wanatubu, wanakimbilia madhabahuni huku wameinua mikono yao, wakilia wapate rehema, na kanisa lote zima ni mwali wa moto, likiwa na utukufu wa Mungu.

⁷⁶ Shauku yetu ya kupata nafasi kuyafanya madhehebu yetu yakue, tumejenga mashule makubwa kuwaelimisha wahudumu wetu, na kuwapeleka mbali na Mungu kuliko walivyokuwa hapo mwanzo. Mungu hajulikani kwa elimu. Hajulikani kwa theolojia. Mungu anajulikana kwa imani. Huwezi kumwelezea Mungu. Yeye haelezeki.

⁷⁷ Angalia kile jambo hilo limefanya, sisi Wapentekoste tuliokuwa wapentekoste. Wanawake wetu wamekata nywele zao; wakijipodoa. Wanaume wetu wanaruhusu hilo. Wahudumu wetu wanaliruhusu. Wanaogopa kusema neno juu yake. Kanisa litawafukuza wakifanya hivyo. Loo, kama hatuhitaji kusafisha nyumba, tangu mimbarani hata kwenye chumba cha chini. Ni aibu. Ni fedheha.

⁷⁸ Watu fulani walinijia, si muda mrefu uliopita, na kusema, “Ndugu Branham, watu wanakupenda.” Lakini kasema, “Wewe

daima unawakemea, unawakemea hao wanawake, juu ya kuwa na nywele fupi na mambo kama hayo.”

Nikasema, “Biblia ilisema ni aibu kwa mwanamke kuwa nayo.”

⁷⁹ Anamwaibisha mumewe anapofanya hivyo. Na ni ishara madhubuti ya kwamba umemwacha Mungu. Kumbuka, katika kisa cha Samsoni, nywele ndefu ilikuwa ni ishara ya Mnadhiri ya kwamba ameuacha ulimwengu, akaingia katika Neno la Mungu. Basi mnapokata nywele zenu, enyi wanawake, mnakataa kwamba ninyi ni ishara ya Kinadhiri. Mmeenda Hollywood badala ya kurudi kwenye Biblia. Biblia ilisema, “Na wasikatwe nywele.” Mnaona, ni aibu na wahudumu hawasemi neno juu yake.

⁸⁰ Mtu huyu akaniambia, “Mbona huwaachi hao wanawake peke yake?” Kasema, “Wao wanakuchukua kama nabii.”

Nikasema, “Sikusema kamwe mimi ni nabii.”

⁸¹ Kasema, “Wao wanakuchukulia hivyo. Wafundishe namna ya kupokea vipawa vya rohani na kufanya jambo fulani. Inakupasa kuwafundisha mambo makubwa, mambo makuu.”

⁸² Nikasema, “Nawezaje kuwafundisha hesabu za mafumbo na huku hata hawatajifunza ABC zao, jinsi ya kuishi maisha mazuri? Utafanyaje jambo hilo? Naam, rudi kwenye jambo la kwanza.”

⁸³ Mwaka baada ya mwaka, nikipita nchini, na inazidi kuwa baya zaidi wakati wote. Kuna kasoro mahali fulani, si na Neno. Si ajabu hatuwezi kuiwasha mioto ya ufufuo. Tunahitaji wakati wa kusafishwa kwa nyumba. Mungu hatafanya jambo hilo kamwe mpaka tutakaporudi tena. Tunahitaji wakati wa kusafishwa kwa nyumba.

⁸⁴ Nawe mwanamume, utamwacha mkeo afanye jambo kama hilo, avae kaptura! Hao si Wamethodisti, Wabatisti. Hao ni Wapentekoste, hiyo ni kweli, “mfano wa utauwa, Wakati wa Kanisa la Laodikia, lenye vuguvugu,” la Pentekoste kwa jina, hivyo tu. Pentekoste si jina, ni tukio la ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaowasafisha watu. Si ajabu hatuwezi kuwa na ibada kubwa za kuponya na kadhalika, kuna kitu kilichoenda kombo mahali fulani. Ni Shetani, aliyetuona huko nje tukijaribu. . .

⁸⁵ “Vema, tukisema kitu juu ya jambo hilo, wao watabadilisha ushirika wao.”

⁸⁶ Kumbuka, huwabembelezi Wakristo. Wakristo wanaparuzi. Wao ni wanaume na wanawake wa Mungu, wanaomtetea Mungu, haidhuru mtu mwingine ye yote atasemaje. Haikubidi kuwasihi na kuwashawishi, na kuwapaka manukato na kuwabembeleza kila mahali. Hiyo ni mimea ya tuta, mimea ya kisasa, haifai kitu katu, haitazaa kitu.

⁸⁷ Inanikumbusha, kama . . . Hivi karibuni itakuwa ni wakati wa kuatamia. Niliwaona ndege wadogo leo, kule, shoromo wadogo wakipeleka nyasi kwenye viota vyao. Haitachukua muda mrefu kabla hawajaanza kuatamia, kuviangua vijiyai vyao. Mnajua, ndege mdogo anaweza kuwa kiota cha mayai, naye anaweza kuketi kwenye kiota hicho cha mayai, naye huyageuza kila baada ya dakika chache; anachukua vijiguu vyake na kuyageuza, na kuketi pale. Sasa, akiyaacha hayo mayai yapate baridi, baada ya kuyapasha joto, hayataangua. Naye anaruka tu na kupata mego moja la chakula, anarudi haraka anayakalia tena.

⁸⁸ Nanyi mwajua, maskini mama ndege huyo, angeweza kuketi pale kwenye mayai hayo, na kuyageuza kila dakika mbili, na bila . . . hata ajitolee na kufunga hata awe mdhaifu sana hawezi kutoka kwenye kiota. Lakini isipokuwa, basi, ya kwamba mama ndege huyo amekuwa pamoja na ndege wa kiume, hayo mayai hayataangua. Haidhuru nini, hata ungeyabembeleza vipi, hayataanguliwa. Yatakaa moja kwa moja kwenye kiota na kuoza.

⁸⁹ Na kama kulipata kuwa na wakati ambapo Pentekoste inapaswa kuwa na Mwenziwe, Yesu Kristo; maana hatupati kitu ila kiota kilichojaa mayai yaliyooza, wakikana Imani, kuingia katika Baraza la Ekumeni, na kukuita mambo makuu, kuketi kando ya papa, na kusema eti ni “jambo la kiroho.” Una nini kweli, ewe Mpentekoste? Hivi hamjui Biblia ilisema kwamba mambo hayo yangetukia? Nasi tunashangilia ati kwa sababu Wamethodisti na Wabatisti wanaingia, halafu mambo haya mengine yote namna hiyo. Hivi hamtambui ya kwamba mwanamwali aliyelala alipokuja kununua Mafuta, hiyo ilikuwa ndiyo ile saa hasa ambayo Bwana Arushi alikuja? Nao hawakupata Mafuta! Mwajua, Kunyakuliwa kutakuwa kwa siri sana, na kule kuondoka, moja ya nyakati hizi, hata hamtajua hilo linatukia. Mambo yataisha, nanyi mtashangaa imekuwaje.

⁹⁰ Kama vile Yohana alivyokuja duniani. Nao wakamwambia, kasema, “Vema, Biblia ilisema, imempasa Eliya kuja kwanza.” Yeye akasema, “Yeye amekwisha kuja, msimjue.”

⁹¹ Ndivyo itakavyokuwa, siku moja, wao watasema, “Nilifikiri hili lilipaswa kutokea kabla ya ule wakati wa ile Dhiki kuu. Nilifikiri Kunyakuliwa kulipaswa kutukia.” Maneno yanaweza kujibiwa, “Imetukia tayari wala hukujua.” A-ha. Huenda ikawa imechelewa kuliko unavyodhania. Loo, amkeni, enyi kanisa! Afadhali niache hilo; sikuja hapa kwa ajili ya fundisho, nilifikiri ningesukumiza hilo kusudi tu mwe na hilo pembeni.

⁹² Kumbuka, ndugu, Shetani ameona mipango hii mikubwa, kanisa moja likijaribu kulishinda jingie, madhehebu moja yakijaribu kuyashinda mengine, kung’oa ujinga wote na inawabidi kuwapa mtihamu wa saikolojia, kumleta

mwanasaikolojia amjaribu mtu kabla hajaingia katika kazi ya kimishenari. Pentekoste! La, hao—hao—hao si Wapresbiteri, hao ni Pentekoste. Mtihani wa saikolojia unahitajika kwa kundi fulani la Wapentekoste, kundi kubwa, kabla wamishenari hawajaingia kazini.

⁹³ Vipi kama walikuwa na mtihani kama huo? Wao wana mtihani. Ulikuwa mtihani wa kipentekoste mwanzoni, walipongojia kwenye chumba cha juu mpaka ukaja Moto kutoka Mbinguni, na Nguvu za Mungu. Mtihani ulikua ndio huo.

⁹⁴ Si mwanasaikolojia wa kidunia, nusu mlevi amesimama pale akijaribu kufanya bongo lichenke, ama jambo fulani, aseme, “Wewe umekwisha kabisa.” Wakati, imethibitika kabisa ya kwamba mtu wa kiroho sana huwa ana wasiwasi, anapaswa kuwa katika hali hiyo apatae kuingia Mle. Kwa hiyo haya basi, unaona, na kuharibu tu kile Mungu amejaribu kufanya kwa miaka mingi, na kurudi moja kwa moja wakiwa na mipango yao na ninii yao kuu. . .

⁹⁵ Wanafurahi wakiona watu wengi sana wamekusanyika pamoja. Husema, “Laiti ningaliweza kuwafanya wote Wamethodisti!” Wamethodisti wanajaribu kuwafanya wote hao Waassemblies! Laiti ningaliweza kwafanya wote hao wa Umoja! Laiti ningaliweza kuwafanya wote Wamethodisti, Wabatisti wanajaribu kuwafanya wote Wabatisti, Wapentekoste wote Wapentekoste! Loo, huwezi kufanya kitu juu yake, Mungu amewachagua hao tangu kuwekwa misingi ya dunia. Hatuna budi kuhubiri Injili. Hivyo tu. Lakini, mipango yetu mikubwa, tumeondoka bila Moto huo. Tumeondoka na kujiwashia moto wa kujitengezea, kama tusemavyo.

⁹⁶ Na ukomunisti wetu, sasa tunaogopa sana, ukomunisti umeingia, “Itakuwaje?” Lakini, mwajua, jambo muhimu si ukomunisti. Hebu niwaambie jambo hilo sasa, mimi siogopi ukomunisti.

⁹⁷ Bali ninachohofu, enyi Wapentekoste, Baraza hili la Ekumenia litawachukua. Jambo ndilo hilo. Litafanya ile alama ya mnyama, nanyi itawalazimu kuingia mle. Kwa maana ninyi ni madhehebu, itawabidi aidha kuingia au kutoka. Jambo ndilo hilo, na mtu ye yote ambaye ni mwema, mwenye akili, na ni wa kiroho anajua jambo hilo. Tunahitaji ushuhuda mwingine wa baharini, tunaona sasa. Na Wapentekoste wetu, wakiyameza tu, ndoana, ugwe na chubwi, yote kwa jumla, “Jinsi kitakavyokuwa kitu kikubwa.” Wakati, Wamethodisti, Wapresbiteria, Waluteri, kanisa la Kristo, na Wapentekoste, itawabidi kukana—kukana fundisho lenu muhimu la kimitume, mpate kuwa mle. Itawabidi wao kufanya jambo lile lile. Hamtakuwa na uhusiano wo wote nalo. Lote linaungana na Rumi, jambo lile hasa lililothibitishwa. Maandiko yalisema jambo hilo.

⁹⁸ Kuna nini kwa wahubiri wanaoacha mambo haya yafikie hali hii, bila kuwaonya watu? Mungu atawawajibisha jambo hilo. Katika wakati uu huu wa shida, walikuwa shidani, walikuwa na shida. Ukomunisti hauingii; ni Baraza la Ekumenia litakalomeza kundi hilo lote. Pia kumbukeni, mtakaposema, “Wakati litakapotukia,” mmeishachelewa sana wakati huo, tayari mmechukua alama ya mnyama. Ninyi ni mali yake wakati huo.

⁹⁹ Afadhali uende mahali unapoweza kuitoroka sasa, naam, bwana, utiwe muhuri katika Ufalme wa Mungu. Mwili wa Kristo ni Mwili wa kisiri wa Kristo, ambamo wewe unabatizwa ndani Yake na Roho Mtakatifu; si kujiunga Nao, si kuingizwa ndani Yake, si kuzungumziwa hata ukaingia Mle, kunena kwa lugha hata ukaingia Mle, kupiga makelele hata ukaingia Mle. Unazaliwa Mle, kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Bila shaka.

¹⁰⁰ Sasa tunaona mambo haya, shida inaingia mara moja. Loo, Ibilisi aliangalia akasema, “A-ha, wao wameendea madoido, wao wako tu kule wakirukaruka, wakipiga makelele, wakiwa na wakati mzuri sana. Wajua nini, hivi sasa ndio wakati wangu wa kuwazamisha. Nitajilipiza kisasi sasa.”

¹⁰¹ Kwa hiyo akasimama juu ya kilima akaanza kupulizia pumzi yake ya sumu, whii, “Siku za miujiza zimepita. Kwanza, ninaamini watu hawa ni wasiwasi tu. Nafikiri wanapaswa ku—ku—kufanya mtihani wa akili kabla hawajaingia hudumani nchi za ng’ambo.” Wapentekoste! A-ha. Oneni pumzi yake yenye sumu ikiliua Neno, “Loo, nafikiri ni kitu kingine, na—naamini...” Mnaona, mnarudi moja kwa moja kama madhehebu mengine yote yalivyofanya, hiyo hasa ndiyo barabara wanayopitia. Wataipitia, inaua kitu hicho. Saa hiyo hiyo mnapofanya madhehebu, jambo hilo linaliua. Daima huliua. Itakuwa hivyo daima. Halitainuka tena. Jambo hilo halijajulikana katika historia. Katika—katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, Kristo alikuwa nje ya kanisa, akibisha, akijaribu kuingia. Nao hawawezi kulivumilia Hilo. Hawawezi kulisikiliza. Sasa tunaona, saa tunayoishi, shida imeingia.

¹⁰² Halafu tunaanza kuona, miujiza haitendeki tena, kama ilivyokuwa ikitendeka. Wagonjwa wanaenda nyumbani wakiwa wagonjwa. Si kwa sababu ya Mungu. Ni kwa sababu ya ukosefu wa ufufuo kati ya watu. Hakuna ufufuo. Wao-wao wanaketi na kusikiliza; wanaenda nyumbani, wanasema, “Vema, nafikiri huo ulikuwa mzuri sana. A-ha.” Unaona, hakuna ile bidii. Hakuna kitu fulani kile ndani ya watu kinachopaswa kuwa mle.

¹⁰³ Nakumbuka miaka kumi na mitano iliyopita, hapa katika Arkansas, nilipokuwa na mkutano mdogo hapa Jonesboro, wakati yapata watu elfu arobaini walipokuwa wakijaribu kuhudhuria huu, kuhudhuria mkutano kwenye mji wa yapata watu elfu kumi na tano. Nao walilala chini ya magari ya pamba

na cho chote kile, na kuwafunika watoto wao wagonjwa kwa makaratasi, wapate tu kuingia ndani. Waliketi vitini mwao nao wasingeondoka, usiku na mchana, na waliwatuma wapendwa wao kwenda kununua sambusa na chu—chupa ya soda; na kukaa pale, mchana kutwa na usiku kucha, mchana kutwa na usiku kucha. Mioyo yao ilikuwa inawaka, ina moto. Jambo dogo sana alilofanya Mungu, liliwatia moto. Na mamia yao wakaingia.

¹⁰⁴ Yeye angali ni Mungu yeye yule, usiku wa leo, aliyekuwa miaka kumi na mitano iliyopita. Yeye angali ni Mungu yeye yule, usiku wa leo, aliyekuwa wakati alipoumba mbingu na nchi.

¹⁰⁵ Lakini ni kitu gani? Sote tuliona shauku sana na tukataka kujenga madhehebu yetu, tukataka kujenga *hiki* na kujenga *hiki*, na kufanya kitu fulani kikubwa na kinachometameta, kujilinganisha na akina Yahe, na Wamethodisti, na Wabatisti, na Wapresbiteri. Wewe si mmoja wao. La, wewe si mmoja wao. Hao ni watu wa kimadhehebu, jambo ambalo ni sawa, sina neno juu yao. Kuna Wakristo wengi wazuri kati yao, bali hupaswi kujihusisha na makundi hayo yasiyoamini. “Watu wanaokataa Nguvu zake,” hampaswi kuungana nao.

¹⁰⁶ Mnajua, shida yake ni, mnajaribu kuingiza Hollywood kanisani. Jambo mnalopaswa kuwa mkijaribu kufanya ni kuondoa Hollywood kanisani. Mnaona? Mnajaribu kulifanya jengo lenu zuri sana, mnajaribu kuyafanya madhehebu yenu makubwa sana, hata yatawavutia watu. Hatuwezi kwenda upande wao. Hatuna budi kuwaleta upande wetu. Kila kitu kinachometameta, kumbuka, Hollywood humetameta kwa anasa za duniani, wakati Injili inameka kwa upole. Kuna tofauti kubwa kati ya kumetameta na kumeka. Injili humeka kwa upole, na unyenyekevu, na uadilifu, na nguvu. Wakati, Hollywood humetameta, na kila mtu akishangilia na kupiga makelele, na kuiendea. Mnaona? Hatuhitaji jambo hilo.

¹⁰⁷ Tunataka kuishi Nuru ya namna hiyo. Yeye alisema, “Ninyi ni chumvi ya dunia.” “Kama chumvi ikiharibika,” yaani ni nguvu zake katika Injili. Tunapaswa kuwa na kitu fulani kikiendelea makanisani mwetu, mpaka Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, na hao wote, wangetamani sana kuja. Tunapaswa kukolea! Chumvi husababisha kiu, huleta kiu. Chumvi ina ladha, ikilambwa. Haina budi kulambwa.

¹⁰⁸ Nasi tunaona, madoido yetu makuu kujaribu kujilinganisha na Methodisti na Batisti, pamoja na majengo makubwa na mahali pakubwa, na watu wazuri wenye elimu, na mashule makubwa na vyuo vikubwa zaidi, na kila kitu namna hiyo. Tumepotea katika madoido, na hapa shida imeingia.

¹⁰⁹ Nao moyo wa kiroho unaangalia kila mahali na kusema, “Hebu, ngoja kidogo hapa, sisi sote itatulazimu kujiunga na Baraza hilo la Ekumeni? Hivi kundi letu lote litaingia mle?” Hakika, mtaingia. Hiyo ni kweli kabisa. Angalieni mwone

kama hamtaingia. Biblia ilisema mtaingia, kweli kabisa, Naye Kristo angekuwa nje. Mwezi ulifanyika giza mbele ya papa (wa kwanza aliyepata kwenda Rumi), juzijuzi usiku, ukiwaonyesha ishara mbinguni. Bila kutarajiwa, ulitiwa giza. Jinsi Bwana anavyofanya mambo katika siku hii, ajabu sana!

¹¹⁰ Ndipo katika saa hii kuu yenye giza, walipokuwa kule, upepo ukavuma. Matumaini yote ya kupona yamekwisha. Sasa utafanya nini kama madhehebu yako yakiingia katika Baraza la Ekumeni? Itakuwaje basi kwa vitu vyetu vyote vikuu ambavyo tumejenga hapa duniani, matumaini ya mwisho yamekwisha!

¹¹¹ Lakini mnajua, walipokuwa karibu kupiga mayowe, na matumaini yote yamekwisha, wasingeweza kuokolewa; na mara, wakamwona Yeye anakuja, akitembea juu ya maji. Katika saa yenye giza, Yeye alikuja, anatembea.

¹¹² Mnajua nini? Alipowaacha, Yeye alijua jambo hilo litatukia, kwa hiyo akapanda kilima kilicho kirefu kuliko vyote kilichokuwamo nchini. Jinsi unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Basi akapanda kusudi aweze kuwaona, mwajua.

¹¹³ Naye alijua jambo hili lilikuwa linakuja. Alitabiri siku hii ya leo itakuja. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu anafunuliwa.” Basi, Mwana hana budi kufunuliwa. Kizazi hiki kibaya na cha zinaa kitatafuta ishara. Kitapata ishara. Kitaikataa kama walivyofanya wakati huo, bali itakuwa ni ishara ya ufufuo. Yeye yungali hai, akitenda kama alivyotenda.

¹¹⁴ Tunaona, ya kwamba katika saa hii kuu, hao wanafunzi wote wakihangaika, Yeye alipanda juu kusudi aweze kuwaangalia. Yeye alikuwa ameketi kule juu kilimani, akiwaangalia.

¹¹⁵ Na sasa Yeye hakupanda mlima fulani wakati huu, bali alipanda kutoka kaburini, akapanda kupita hewa, akapita mwezi, nyota, hata akapanda juu sana mpaka inambidi kuangalia chini apate kuona Mbinguni. Naye huyo pale ameketi, Juu. Sasa macho yake yanamwangalia shomoro, nami najua Yeye anatutazama. Anatutazama.

¹¹⁶ Na papa hapa katika saa hii yenye giza, wakati makanisa yote yameingilia miradi mikuu, nao wana mradi *huu* na maradi *ule*, yote imepangwa jinsi makanisa mengine yamefanya, madhehebu. Basi jambo gani limetukia? Katika saa yenye giza, wakati watu waliojazwa na roho kweli wanashangaa, “Itakuwaje? Waangalie watoto wangu!” Mwanamume anasema, “Mwangalie mke wangu! Angalia jambo *hili!*”

¹¹⁷ Nao wanamaliza mkutano wa maombi ya Jumapili, ama ya Jumatano usiku, mapema, ili waweze kwenda na kuangalia kipindi cha *Tunampenda Sacy*, ama kitu kama hicho, kwenye

televisheni. “Wanaoupenda ulimwengu, kuliko kumpenda Mungu.” Kutenda kama wao.

118 Nilimwambia bibi fulani juzijuzi, alikuwa amevaa nguo iliyombana sana. Nikasema, “Dada, nguo hiyo inabana sana. Huenda isisikike sawa kwangu kukuwambia hivyo, bali imebana. Wewe ni Mkristo, nawe ungeweza kuweka jiwe la kujikwaa.”

119 Akasema, “Vema, Ndugu Branham, unajua nini?” Kasema, “Wao hutengeneza za namna hii tu.”

120 Nikasema, “Wangali wanauza jora, na wana vyerehani. Hakuna udhuru.” Naam.

121 Sikilizeni, hebu nikwambie jambo fulani, rafiki yangu mpendwa. Si kukukemea. La, bwana. Ninajaribu kukuempusha na yale mateso. Mradi tu roho hiyo ingali ndani yako, utafanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Huna budi kuzaliwa toke kwake. Sasa unaweza kujiridhisha kwa tamshi hilo, lakini hebu nikwambie jambo fulani, unaona, “Moyo wako ulipo, ndipo itakapokuwepo na hazina yako.”

122 Hebu nikwambie. Unaweza ukawa msafi sana kama yungiyungi kwa mume wako, na unaweza kuwa msafi tu kama yungiyungi, ewe msichana, kwa rafiki yako mvulana, lakini siku moja Mungu atakufanya uwajibike kwa ajili ya kufanya uzinzi. Una hatia unapovalia namna hiyo. Yesu alisema, “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Basi itakapombidi mtu huyo kujibu, huyo mwenye dhambi, kwa kukuangalia, kwa kuzini, ni nani aliyejianika kwake? Wazia jambo hilo. Enyi wanawake wa Kipentekoste, hamna haya! Mnaona? Hamna haya!

123 Ninawapenda, hiyo ndiyo sababu ya kusema jambo hilo. Upendo husahihisha.

124 Tunafanya madoido makubwa, madoido makubwa ya nguo. Ni kama tu, na inafanana na, ulimwengu. Yeye alisema, “Msiipende dunia, wala mambo yaliyo katika dunia; kama mkiipenda, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yenu,” sijali unanenaje kwa lugha, unarukaruka, unacheza; unakata nywele, unavaa nguo kama namna hiyo. Ninyi wanaume mnaruhusu jambo hilo. Matunda yenu wenyewe yanawaambia mliko. Hiyo ni kweli kabisa. Si ajabu tuko katika machafuko tuliyomo, na pepo za ukomunisti, pepo za ukanisa, pepo za shirika la ekumeni.

125 Ni—ni wakati wa kujiunga, wakati wa muungano. Mashirika yanaunganisha wafanya kazi, wakizozana juu ya jambo hilo. Mataifa yana U—Umoja wa Mataifa, yanaungana. Makanisa yanaungana pamoja. Yote yanaonyesha kitu gani? Inaonyesha ya kwamba Kristo na Bibi-Arui wako tayari kuungana. Hilo ndilo yanavyoamaanisha. Vivuli hivyo vyote vya vitu vinaonyesha

kitu halisi kinachokuja. Angalieni sasa tunapofunga, maana ninachelewa sana.

¹²⁶ Basi sasa angalia, katika saa hiyo kuu wakati matumaini yote yalikuwa yamekwisha, ya kupona, walimwona Mtu fulani akija, anatembea juu ya maji, akiwakaribia. Na jambo hilo, jambo la kuhuzunisha, sikilizeni kwa makini, kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa. Walisema, “Kinaonekana kama kivuli. Huenda ikawa, wajua, ni kivuli.”

¹²⁷ Kama jambo hilo halijatukia tena! Wanaiogopa Hiyo. Wanaogopa kupiga ramli, mnaogopa namna fulani ya nguvu za ibilisi; wakati Yesu alisema Hilo lingetukia katika siku hii. Kitu tu kinachoweza kuwasaidia ni Yesu Kristo. Si madhehebu mengine, si yote kuungana pamoja, hilo litayafanya yawe mabaya kuliko zamani. Kitu tu kinachoweza kukusaidia ni Yesu Kristo.

¹²⁸ Na wakati alipoahidi kurudi katika siku za mwisho, katika hali hii, na kufanya jambo hili, akamwahidi (kabla tu ya yule mwana aliyeahidiwa kumrudia Ibrahimu, mzao wa kwanza) mzao wa kifalme wa Ibrahimu, Yesu angeninii... kasema tungeona jambo lile lile. Kabla ya Mwana aliyeahidiwa, Mungu angejidhihirisha Mwenyewe katika mwili na kufanya sawasawa kabisa yale Yesu aliyofanya, kama Yeye alivyosema Yeye angefanya, kama alivyosema ingetendeka katika siku za mwisho. Na hizi hapa ahadi hizo zote, ambazo tungeweza kuziorodhesha, kwa madazani, papa hapa mbele yenu, ya kwamba jambo hili linapaswa kutukia.

¹²⁹ Nayo makanisa, ambayo yanapaswa kunyosha mikono yao, kuipokea Hiyo, “Kidogo ninahofu Hilo. Si la kundi letu, unaona.” Nalo linawafadhaisha. Kitu pekee kinachoweza kuwaleta kwa Kristo, ni Kristo Mwenyewe, nao wanahofu kwamba kinatisha. “Loo, sijui. Hicho kinaweza kuwa ni kivuli, mnaona. Nami sijui habari Zake.” Wanaogopa kitu pekee kinachoweza kuwasaidia.

¹³⁰ Na katika saa hiyo yenye giza na dhiki, hilo kanisa lililochaguliwa, kundi hilo lililoketi pale nje, likihofu kwamba huenda ikawa ni kivuli, hawakutaka kujihusisha na jambo hilo. Ndipo ikaja ile Sauti tamu, “Msiogope. Ni Mimi.”

¹³¹ Yeye ni Neno. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye habadiliki, kuwa Neno. Sasa hamwezi kusikia Neno likisema, usiku wa leo, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Msiogope; ni Mimi?” [“Amina.”]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹³² Baba wa Mbinguni, ji—jioni hii ina joto. Majira yana giza, jinsi Moto umepoa madhabahuni. Unaokota masazo ya wavunaji shambani. Wewe ulisema, “Ufalme umefanana na mtu aliyechukua jarife akaenda baharini, akaitupa ndani, na wakati alipoivuta. Ufalme ulikuwa namna hiyo.” Bwana

Mungu, siku moja, huyo samaki wa mwisho aliye majini! Wewe ulisema, “Walichukua wa kila aina.” Jarife hiyo ya Injili hushika wa kila namna; ilishika kasa, kamba wa mtoni, buibui, nyoka, samaki topasi. Hatujui inashika kitu gani, bali kulikuweko na samaki mle uliokuwa ukiwatafuta Wewe. Wewe ndiwe Hakimu. Bali tunatambua, upesi kasa, kamba wa mtoni, na kadhalika, wananarudi kwenye mashimo ya matope tena, wananarudi majini. Bali siku moja huyo samaki wa mwisho aliyechaguliwa, aliyechaguliwa tangu zamani kuja, ile sehemu ya mwisho ya ule Mwili, itatolewa kwenye ziwa hilo.

¹³³ Ulitupa jarife katika siku za Luther, na Wesley, Alexander Campell, John Smith, Calvin, Knox, Finney, Sankey, na kadhalika; katika wakati wa Kipentekoste, siku za F.F. Bosworth, na Frochman, hao watu mashuhuri. Ulitupa jarife, katika siku za Billy Sunday, kote kote katika nyakati.

¹³⁴ Na sasa ungali unatafuta baharini. Kuna mmoja wao anayeketi hapa usiku wa leo, Bwana? Kama yupo, naomba wawe kama maskini mwanamke yule kisimani. Hata katika hali yake ya umalaya, yeye angali alitambua ya kwamba Wewe ni Masihi. Aliona ile ishara. Hiyo ilitosha. Akasema, “Natambua kwamba Wewe ni nabii.” Hakuwa na habari ya kwamba huenda ikawa ni Masihi. Alisema, “Tunamngojea Masihi,” katika maneno mengine. “Tunajua Masihi ajapo, atatwambia mambo haya.” Nawe ulisema, “Mimi Ndimi.” Hiyo ilitosha.

¹³⁵ Sasa, usiku wa leo, Bwana, hebu waone jambo hilo, “Ni Mimi; msioCOPE. Ni ahadi Yangu.” Waponye wagonjwa, Bwana, waokoe waliopotea, wajaze walio tupu.

¹³⁶ Jalia tuondoke usiku wa leo, na tuseme mioyoni mwetu, tunapoondoka, kama hao waliotoka Emau, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akituhudumia usiku wa leo jengoni, Uwepo Wake wa Kiungu!” Jinsi walivyojua ilikuwa ni Wewe, walikualika Wewe uingie ndani ndipo macho yao yakafunguliwa. Jalia kila mmoja wetu, usiku huu, akualike ndani. Kama hatufahamu jambo Hilo, jalia tukualike uingie, hata hivyo. Hivyo ndivyo tu unayoweza kujifunua Mwenyewe.

¹³⁷ Nasi tunaona jinsi ulivyojifunua Mwenyewe baada ya kufufuka Kwako, ulifanya jambo fulani kwa njia ile ile uliyofanya kabla ya kusulubishwa Kwako. Sasa njoo usiku huu, Bwana, Wewe ulisema ni Wewe “yule jana, leo, na hata milele.” Fanya tena, kwa ajili yetu, kama uliyofanya katika siku zile uliposimama hapa katika mwili, duniani. Tutaenda nyumbani, wenyewe mioyo yenye furaha, kama hao. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

¹³⁸ Sasa katika ibada, usiku wa leo, najua kuna joto sana, nasi tuna dakika ishirini kutoka katika wakati mzuri. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Mimi . . .

139 Siwezi kukomesha wala kuzuia mambo ninayofanya. Ninaongozwa na kitu Fulani, daima nimeongozwa, maishani mwangu mwote, na daima kimekuwa sahihi. Hakijaniambia kitu ila kile kilichokuwa kwenye Biblia. Siwezi kukizuia. Siwezi kufanya kitu juu yake. Kinafanya hivyo tu, haidhuru. Nami nina hakika, kama nikiwa mwaminifu, kulikuwa na mtu aliyekihitaji. Nami nitakuwa mwaminifu. Na kwenye Siku ile, ninataka kuninii, kama yule Mtakatifu mkuu Paulo alivyosema, “Hakuna damu ya mtu ye yote iliyi mikononi mwangu.” A-ha. Na—nataka kuwambia Kweli. Si jinsi nilivyo. . . Ninawapenda.

140 Na kama ulikuwa na mvulana mdogo. . . Sasa fikiria jambo hilo, bibi, ninyi ambao niliwakemea muda kidogo uliopita, ninyi akina dada mliokata nywele zenu na kadhalika. Kama mimi. . . Kama ulikuwa na mvulana mdogo aliyeketi kule nje barabarani, nawe ukasema, “Kadogoo, kipenzi, afadhali uingie, kipenzi. Huenda ikawa, sijui, labda watakukanya-kanyaga.” Humpendi mtoto huyo. Hiyo ni kweli. Utatoka uende kule umpige kwelikweli, ama umlazimishe aingie. Hiyo ni kweli. Unampenda.

141 Hivyo ndivyo Injili ilivyo. Mungu anakupenda. “Na hao ambao anawapenda, Yeye huwarudi na humpiga kila mwana amkubaliye.” Kama hamwezi kuvumilia marudio, mnaondoka na kukasirikia jambo hilo, basi ninyi ni watoto haramu, ninyi si watoto wa Mungu. Kwa hiyo kumbukeni tu, ni Maandiko tu.

142 Sasa neno moja kutoka Kwake, neno moja, litamaanisha zaidi ya yale ningeweza kusema, nyakati milioni moja za muda wa uhai. Ni Yeye. Tunajua ahadi Yake. Tunajua alichohidi kufanya. Sasa sijui kama. . . je! . . . tutaninii kutoka. . .

143 Je! alisambaza kadi za maombi tena? Ulisambaza kadi za maombi leo? Ilikuwa nini? J, vema. Vema, kuokoa wakati, hebu tuanze tu na namba moja. Sasa, labda wako kila mahali jengoni. J, namba moja.

144 Na sasa tumetawanyika. Tulianza kutoka, wakati mmoja, kutoka kwenye *hii*, kwa muda, huku na huku, na kila mahali, lakini wakawa wametapakaa kila mahali hapa. Bali kila watu wanoingia, kila siku, wana nafasi ya kuingia mstarini. Hiyo haimaanishi ati kwa sababu uko hapa. . .

145 Ni wangapi wanajua, katika mkutano huu, kumekuwa na karibu mara mbili walioponywa wakiwa katika wasikilizaji, kama walioponywa wakiwa hapa? Hakika, mwajua jambo hilo. Mnaona, kadi ya mombi ni ya kuwaleta tu watu hapa, wapate kuwa na Roho Mtakatifu kati yao, maana mmezoea kufanya jambo hilo. Hata si lazima tuwe nayo sasa. Tunaweza kuacha kadi za maombi.

146 Kama tu tulivyofanya jana usiku, hatukuwa na kadi za maombi jana usiku. Roho Mtakatifu alienda kati yao hao wasiokuwa na kadi za maombi. Nami niliona mambo mengi

ambayo sikusema kitu juu yake, kwa maana sikujua kama ilikuwa ndivyo ama sivyo. Ilizidi kuwa giza juu yao, nami nikaachilia jambo hilo tu. Sikujua. Haingalifaa kitu kuwaita. Lo lote analosema ni kweli, kwa hiyo sikilizeni asemalo Yeye.

¹⁴⁷ Sasa ulisema hiyo ilikuwa ni J? J, namba moja. J, namba moja, ni nani aliye na kadi ya maombi, inua mkono wako. Lazima umekosea, mwanangu; lazima iwe ni baadhi. . . Loo, nasikitika. Loo, kule nyuma kuegemea ukuta kule nyuma. Njoo hapa, bibi. Wao—wao wanaleta tu kadi hizi sasa, yule mvulana, Ndugu Borders ama Billy, mmoja wao, wakati mwingine wote wawili, wanazichanganya hizo kadi mbele zenu, kisha wanakupa kadi yako, yo yote unayotaka. Hutujui, wao tu. . . *Huyu* huenda akapata namba tano, na *yule* apate namba saba, *huyu* apate namba kumi na tano, na *yule* tisini na tano, nasi hatujui. Halafu, tena, ninapokuja, mimi huninii tu, po pote ninapoongozwa moyoni mwangu, naita kuanzia hapo, hata iwe ni wapi. Naninii tu. . . Kama nikisema. . . Wakati mwingine ninahesabu ni wangapi walio kwenye safu, na kuwagawanya na wale walio kwenye safu hii na kupata jawabu. Mnaona? Halafu basi, kama sifanyi jambo hilo, mbona, nina ninii tu. . . yo yote inayonijia moyoni mwangu kwanza, ninaiita.

¹⁴⁸ Namba moja. J, namba mbili. Namba mbili, namba tatu, namba nne, namba tano, namba sita, saba, nane, tisa, kumi, hebu waje, mnaona. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Hilo ni zuri. Hivyo ndivyo ilivyo, njoni moja. . . Ngojeni, mmoja alienda upande ule mwingine. Nilikuwa. . . Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Sawa. Sasa, hapa, hii hapa, kumi. Sawa.

¹⁴⁹ Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Hao ni watano zaidi. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Sawa, hilo ni sawa.

¹⁵⁰ Kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Moja, mbili, tatu, nne. Ninaona tu wanne. Ishirini, ishirini iliitikia? Sawa. Sasa, hatutaki kuwafanya wengi sana kusimama wakati mmoja. Sasa kama tukiwamaliza hawa, ni mapema vya kutosha, tutawaita wengine. Hatuiti. . . Labda sisi. . .

¹⁵¹ Hebu tujaribu wengine wachache. Hebu tujaribu watano zaidi. Ishirini na moja mpaka ishirini na tano, kwenye za J, hebu wasimame tafadhalini. Ishirini na moja mpaka ishirini na tano. Moja, mbili, tatu, kule nyuma kabisa, nne. Moja, mbili, tatu, nne, hao ni watano. Sawa, sasa hebu tuachie tu hapo. Kuna ishirini na watano msitarini, nao wana—wanafanya mstari hapa chini.

¹⁵² Sasa nitawasihi kitu kimoja. Tafadhalini nisikilizeni kwa ninii sana. . . Msikilize Mungu kwa makini sana, kwa dakika zingine kumi na tano, kumi na sita. Mtafanya hivyo? Na mtafanya jambo hili, kuifungua mioyo yenu? Sasa

kumbukeni yale niliyosema. Msilisahau jambo hilo, kama maji yanayotiririka mgongoni mwa bata, kama wahenga walivyosema. Msifanye jambo hilo. Fikiria jambo hili.

¹⁵³ Kama nikiwaambia jambo lo lote lisilo kwenye Maandiko, na ahadi ya wakati huu, una jukumu la kumwona meneja hapa naye aje aniambie. Sawa. Mimi—mimi sifundishi jambo lo lote isipokuwa lililo kwenye Neno. Nami kama nikidumu sawasawa na Neno hilo, na kama nikisema ndivyo lilivyo, naye Mungu . . . Liko kwenye Biblia. Kama Malaika wa Bwana aliniambia jambo fulani ambalo halikuwa katika Biblia, isingekuwa ni Malaika wa Bwana. Hiyo ni kweli. Hajapata wakati mmoja kuniambia jambo lo lote ila lile lililokuwa kwenye Neno hilo, nanyi mnanishuhudia. Yeye kamwe hajasema jambo moja, kati ya mamia ya maelfu na maelfu, na lugha za ulimwengu, Yeye hajasema jambo lo lote lililo makosa, wala kusema lo lote ambalo halikutimia.

¹⁵⁴ Sikilizeni. Mwulizeni menaja na hao wengine hapa. Haya mnayoyaona ninyi nyote hapa, ni madogo tu ya yale mengine. Hiyo ni kweli, ndugu zanguni? [Ndugu wanasema, “Ni kweli.”—Mh.] Mbona, huko nje, na huko nje katika maisha ya faragha, ambako Yeye husema, “Shuka uende mahali *hapa*, ukamwone *huyu*. Na jambo *hili* litatimia. Kisha usema *hivi* mahali hapa, *hapa* chini.” Inaendelea tu, daima, mnaona, mwaka rudi mwaka nenda. Watu kwenye kusanyiko wanaona tu ma—mambo madogo. Lakini sasa kama mtakuwa wenye uchaji.

¹⁵⁵ Sasa kila mtu aliye kwenye mstari wa maombi, waliosimama hapa, ni wageni kwangu? Inueni mikono yenu kama ninyi ni wageni kwangu. Vema. Wangapi huko ni wageni, wanajua ya kwamba sijui kitu juu yenu? Inua mkono wako. Sasa wakati . . . Asante. Sijali mahali ulipo, kama uko juu kwenye roshani, anagemea ukuta, *hapa* chini, hata uwe wapi. Nita- . . .

¹⁵⁶ Sasa, hii ni kwa faida yenu. Hili ni kwa manufaa yenu. Mnaona, hili ni kwa manufaa yenu.

¹⁵⁷ Nilifikiri huyo alikuwa mjukuu wangu mdogo anazungumza nami basi, lakini siye. Nina mjukuu mdogo hapa ndani mahali fulani, usiku huu, yeye ni mrefu hivi, nami nilifikiri ilikuwa ni mtoto Paulo. Yeye daima amesema atakuja, asimame jukwaani, anisaidie kuhubiri, naye bado hajafikia umri wa miaka miwili. Nafikiri mvulana huyo mdogo anamtafuta mamaye.

¹⁵⁸ Kwa hiyo, kumbukeni, mimi ninajaribu kuwasaidia. Mimi. . . Mungu anajua jambo hilo. Ninajaribu kuwasaidia, mnaona. Sasa angalieni, ninataka mfaidike, kama Yeye akija kati yetu.

¹⁵⁹ Sasa kumbukeni jambo hilo, Utu wa Yesu Kristo ukitenda kazi katika mwili, kama Yeye alivyoahidi angefanya mwishoni. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye aliahidi jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama tu ilivyokuwa

kule chini Sodoma, wakati yule Malaika aliyekuwa amegeuza mgongo wake, na ninii . . . Huyo alikuwa ni Mungu. Mnaamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu? [“Amina.”] Hakika, ndivyo ilivyokuwa. Biblia ilisema ndivyo ilivyokuwa. Na Yeye, Yesu, alirejea kwenye jambo hilo. Sasa angalia.

¹⁶⁰ Sasa ninyi huko nje bila kadi ya maombi, ninawatakeni mnifanyie jambo fulani, po pote mlipo. Sasa kumbukeni, mambo haya, angalia wakati Huyo anapokwambia ya kwamba umepona, ama analokwambia ufanye. Angalia yale asemayo. Kama akikwambia tu, hiyo ni kuiimarisha imani yako. Halafu wakati imani yako inafikia kiwango fulani, unanyosha tu mkono na kumkubali Mungu. Si mimi, maana Mungu wa Mbinguni anajua.

¹⁶¹ Ninaangalia kwenye mstari huu hapa, sioni mtu mmoja ninayemjua. Siwezi kuona ila yapata watu wawili watatu katika kusanyiko lote, ninaowajua. Wala sijui kama, sasa hivi, ninaweza kusema, kuonyesha mmoja. Ninajua ya kwamba Edmund Way alikuwa hapa dakika chache zilizopita. Nilifikiri nilimwona, na ni—nikakosa . . .

¹⁶² Kama sijakosea, ninaona mtu ninayemjua, ni mtu na mkewe, na msichana mdogo, jina lake Fritzinger, kutoka huko Ohio. Huyo, je! wewe ni ndugu—Ndugu Fritzinger? Unaketi kwa namna fulani katika duara ambapo . . . Huyo ni Ndugu na dada Fritzinger, kutoka Ohio, rafiki zangu.

¹⁶³ Na nje ya hao, wakiketi kule nyuma, ni . . . nimeona upande huu hapa, ni mzee anayeelekea kwenye umri wa miaka tisini na miwili, jina lake William Dauch. Yeye na mkewe. Yeye ni nesi. William Dauch, huko Ohio, rafiki msiri wangu sana. Si muda mrefu uliopita, yeye alikuwa, umri wa miaka tisini na mmoja, alikuwa na mshtuko mbaya sana wa moyo, ugonjwa wa moyo, naye mkewe akanipigia simu, nije mara moja, alikuwa yuafa wakati uo huo. Na kwenye . . .

¹⁶⁴ Amekuwa rafiki msiri wangu sana. Nilipokuwa ninaenda kumwona, nilihofu. Nami nikasimama, na moja wa ya magurudumu ikaenda kombo, ulikuwa tu unararua tairi yangu vipande-vipande, ndipo nikaenda kwenye kituo cha mafuta kiitwacho Texaco, nikanunua mafuta, nao wakaja, wakauchunguza. Nami nikaangalia juu, nikamwona Ndugu Dauch akitembea kanisani mwangu, akinipa mkono. Nikasema, “Bwana asifiwe.” Ndipo nikaangalia upande *huu*, naye huyu hapa anakuja barabarani, akanipa mkono. Nikaenda kwake.

¹⁶⁵ Nilimwona daktari wake, kijana Myahudi, ama mtu wa makamu, Myahudi mwanamume. Ndipo nikasema, “Vipi kumhusu yeye, daktari?”

166 Akasema, “Ni mahututi kabisa hawezi.” Kasema, “Yuko chini ya hema ya oksijeni.” Kasema, “Atakufa papo hapo.” Akasema, “Kumbuka, yeye ana umri wa miaka tisini na mmoja.”

Nikasema, “Ndio, bwana.”

167 Kasema, “Moyo umeshindwa kabisa. Hakuna liwezalo kufanyika.” Kasema, “Wakati wa kuaga dunia umetimia.”

168 Nami nikasema, “Ndiyo, bwana. Lakini, la, hatakufa. Hivyo tu.”

169 Nikaingia ndani, nikaweka mkono wangu chini ya hema. Nikasema, “Ndugu Dauch, unaweza kunisikia?” Akaniangalia. Sasa kweli, katika jina lake, yeye ni Mjerumani, D-a-u-g-h, nami nalitamka tu Dauch, mnaona. Nami ni—nikaweka mkono wangu chini ya ile hema, na kusema, “Unanisikia, Ndugu Dauch?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Hutakufa. Tayari nimekwisha kuona hufi.”

170 Juma moja tangu wakati huo, nikisimama kanisani mwangu, ni nani anaingia kanisani mwangu ila Ndugu Dauch! Nikaondoka mkutanoni nikavuka mtoni, nikaenda kwenye mkahawa, kula. Basi nilipotoka kwenye gari, nami nilikuwa ninatembea barabarani, huyu hapa Ndugu Dauch anakuja huku amenyosha mkono wake. Maono hayo hayakosei.

171 Na mtu huyo wa miaka tisini na mmoja, naye hufuata kila mkutano, alikuwa California. Waweza kuinua mkono wako, Ndugu Dauch, unayeketi pale, ili watu waone ni askari halisi jinsi gani alivyo sasa. Hapa, akiketi papa hapa, mnaona, umri wa miaka tisini na mmoja, naye hufuata kila mkutano. Ninapokuwa maskanini, yeye huendesha gari maili mia kadha kila siku, kunisikiliza nikihubiri somo dogo, kisha anarudi. Mungu, “Kutakuwako Nuru wakati wa jioni.”

172 Nilisema, juzijuzi nilikuwa nikizungumza naye, nikasema, “Nikufanyie nini, Ndugu Dauch?”

173 “Ombi moja tu, Ndugu Branham. Atakapokuja, nataka kwenda pamoja Naye.”

174 Nikasema, “Usijali. Hilo ni jambo la hakika. Bila shaka.” Sasa, mtu huyo akaja, akabatizwa, loo, akaja na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na kila kitu, ni mtumishi mzuri sana wa Kristo.

175 Sasa nitamwuliza kila mtu, kwa uchaji kabisa, aangelie upande huu na kuomba.

176 Sasa ni waalimu wangapi hapa wanajua ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema, kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Kuhani Mkuu yele yule, Yeye angetenda namna ile ile. Isipokuwa, Yeye, mwili Wake uko kwenye. . . kwenye Kitu cha Enzi cha Mungu.

Ni wangapi wanaojua jambo hilo? ["Amina."] Mwili wa Yesu Kristo uko kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Bali Yeye hutumia miili yetu kujidhihirisha Mwenyewe kwayo, kama tu alivyoahidi kufanya. "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya."

Nitawaomba mketi kimya, mwe na kicho, mkeshe, mwombe.

¹⁷⁷ Sasa, Baba wa Mbinguni, nimejaribu kuwa na kicho tu nijuavyo jinsi ya kuwa nacho, juu ya jambo hilo. Sasa neno moja tu kutoka Kwako sasa, Bwana, halafu naomba ile Sauti ndogo, tulivu, ije kupitia kwa wasikilizaji hawa na kusema, "Ni mimi; msioCOPE." Tujalie, Baba. Nami ninajikabidhi mwenyewe Kwako, pamoja na Ujumbe uliohubiriwa usiku wa leo, pamoja na Neno Lako kuthibitishwa. Haikulazimu kufanya jambo hilo. Bali utalifanya, ama Wewe hutalifanya, kwa maana uliahidi kufanya hivyo. Naomba kwamba Wewe utatujalia jambo hili, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁷⁸ Na kila mtu awe na kicho sana tu, kicho sana tu. U hali gani? Sasa nitawapa Maandiko tunapoendelea. Kama Bwana akifanya, sijui. Lakini tu. . . Nami nimekuwa nikihubiri namna hiyo, mnaona, hiyo ni namna moja ya kutiwa mafuta. Hii ni namna nyingine ya kutiwa mafuta. Hiyo ilikuwa ni baraka tu. Hii, jambo moja tu, linakuchosa sana nusura ufe.

¹⁷⁹ Sasa huyu bibi anasimama hapa. Sijapata kumwona maishani mwangu. Sisi ni wageni? Ninaamini ulisema, muda kidogo uliopita, sikujui wewe. Mungu anakujua. Yeye ananjua. Je! unajua jinsi tunavyosimama hapa sasa, tutawajibika kwa hilo kwenye Siku ya Hukumu? [Dada anasema, "Amina."—Mh.] Unajua jambo hilo? Unajua kile tutakachofanya sasa, Mungu atatuwajibisha kule juu? Nilisema jambo hilo tu kwa kusudi fulani. Sasa, kama Bwana Yesu atanifunulia kile unachofanya, kile kilicho niani mwako, ama kitu kama hicho, ungeamini jambo hilo? Ingekulazimu kuamini jambo hilo, sivyo? ["Amina."]

¹⁸⁰ Mngeamini hilo huko nje, enyi wasikilizaji? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁸¹ Sasa tunasimama kabisa kama yule mwanamke pale kisimani, na Bwana wetu, mwanamume na mwanamke wakikutana kwa mara yao ya kwanza. Mnaona? Haya basi, tukikutana kwa. . . Hiyo ni Yohana Mtakatifu sura ya 4. Sasa kama Roho Mtakatifu atasema. . . Kama uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, kama wewe ni mgonjwa, kama ni shida ya kinyumbani, kama ni shida za kipesa, cho chote kile, sina fununu. Bali Yeye anajua. Lakini anaweza kutambua mawazo yaliyo moyoni mwako. Yeye ni Neno. Mimi siwezi. Mimi ni mwanadamu. Wewe una wasiwasi kidogo tu, na hiyo ndiyo sababu ninafanya jambo hili, unaona.

¹⁸² Hiyo ni moja ya shida zako, ni wasiwasi. Sawa. Na una kisukari pia, hiyo ndiyo shida yako nyingine. Hiyo ni kweli. Matatizo, kuna mambo mengi yameenda kombo. Sivyo?

Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mnaona? Unaamini Yeye atakuponya? [Yule dada anasema, “Ninaamini—Mh.”] Unaamini? Sasa, wasiwasi wako umesababishwa na umri wako, unaona, lakini sasa hayo yote yatakuacha. Nami ninaamini ya kwamba kwa imani tutaenda Kalvari, upate kupewa ile Damu.

¹⁸³ Sasa, hivyo ndivyo alivyofanya hasa. Yeye alimwambia yule mwanamke kisimani shida yake ilikuwa nini. Yake ilikuwa waume wengi kupita kiasi. Yako ilikuwa ule ninii. . . Ilikuwa ni wasiwasi, na shida zako mbili au tatu zaidi. Hiyo ni kweli, sivyo? Hilo ni jambo lile lile.

¹⁸⁴ Sasa, wakati alipomjia Simoni, Yeye alimwambia alikuwa nani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekufanya uamini zaidi? Ingekufanya? Bibi Strong. . . [Yule dada anasema “Stout.”—Mh.] Stout, would you believe? Nenda ukaamini, nawe. . . Yote imekwisha. Amina.

¹⁸⁵ Njoo. Unaamini? Mimi pia ni mgeni kwako. Sikujui wewe. Mungu anakujua. Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kunifunulia mimi shida yako ni nini? Na kama akifanya hivyo, basi Bwana Mungu na abarikiwe. Hiyo ni kweli? [Yule dada anasema, “Naam, ni kweli.”—Mh.] Sasa usi—haikubidi kuhofu, unaona, huyo—huyo ni Yeye, unayemhisi namna hiyo. Vema. Una ugonjwa pia wa hali ya wasiwaisi, wasiwasi wa akili, na unahangaika kwa upesi. Tena una ugonjwa wa kibofu, ini lina kasoro, na una upungufu wa damu. Hiyo ni kweli. Una kitu fulani. . .

¹⁸⁶ Mtu fulani anazidi kutokea hapa. Unaamini Mungu anaweza kukuponya? [Dada anasema, “Ndio, ninaamini.”—Mh.] Kumponya mumeo, pia, na kumpa afya? Unafikiri huo ugonjwa wa tumbo utakuacha, naye atapona? Huo ndio anaougua. Nenda ukamwekee mikono yako, umwambie hivyo, nao uta—utamwacha.

¹⁸⁷ Mimi ni mgeni kwako. Bwana Yesu anatumia sote wawili, sivyo? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Kama Bwana Yesu atanifunulia jambo ambalo. . . kwamba wewe. . . ambalo limo moyoni mwako, unaamini ya kwamba atakuponya? Umekuwa na shida. Una ugonjwa wa—wa—wa nyongo, jambo la kwanza. Na jambo lingine, umeifanya nyongo yako kushikwa na vinonda, lakini hivyo ndivyo daktari wako alivyosema. Sasa, jambo lingine ni, kwamba wanataka kuifanyia hiyo upasuaji. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli? Naam, unaamini ya kwamba Yeye anaweza kuruka jambo hilo? Unafikiri imani yako iko ndani Yake? Sasa wewe unajua huyo si mimi ninayefanya hivyo. Unaamini? Vema. Nenda, na kama ulivyoamini, na iwe hivyo kwako.

¹⁸⁸ Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, nadhani. Bwana Mungu anatumia sisi wawili. Unaamini Yeye anaweza kunifunulia mambo ambayo yangekusaidia? [Dada, “Ndio,

najua.”—Mh.] Wewe, unaamini Yeye atanifunulia. [“Kabisa.”] Ninasema . . . “Kabisa,” hilo ni zuri sana. Hilo ni sawa kabisa. Sasa una shida nyingi, matatizo mengi na kadhalika, na kitu kama kukohoa, nawe huwezi. Na una wasiwasi sana. Na—na hiyo, hiyo ni kweli.

¹⁸⁹ Tena, una mzigo moyoni mwako, na mzigo huo ni kwa ajili ya mtu mwingine, ambaye ni mwanao. Naye ana shi—shida, shida ya kinyumbani. Yeye na mkewe, wao daima wanazozana na kuendelea . . . ? . . . Nawe una mzigo huo. Hiyo ni kweli. Sasa wewe amini kwa moyo wako wote, na hayo yatatoweka na yatakwisha. Sasa amini. Bwana akubariki.

¹⁹⁰ U hali gani bwana? Mimi ni mgeni kwako, nawe—nawe ni mgeni kwangu. Na lime—limeanza . . . Hayo maomo sasa, ninaona, inaonekana kama kwamba nyumba yote inakuwa nuru, kitu kama skisulisuli kikizunguka-zunguka. Mnaona? Lakini unaamini ya kwamba Bwana Yesu angeweza kunifunulia kile kimekufanya usimame hapa? Unaamini angeweza? Ninaamini hilo, pia. Ninazungumza nawe tu, nipate kuipata roho yako, hilo hasa ndilo sababu ya kufanya jambo hili. Mnaona, sikujui, kwa hiyo hapana budi iwe ni kitu kingine mbali na mimi kinachofanya jambo hilo. Sina budi kujiondoa mimi mwenyewe kabisa, kusudi afanye hivyo Yeye Mwenyewe. Unafahamu?

¹⁹¹ Sasa, jambo moja, unaugua ugonjwa mbaya sana wa hali ya wasiwasi, hali hii ya wasiwasi imekuwako kwa muda fulani. Hiyo ni kweli. [Huyo ndugu anasema, “Hiyo ni kweli.—Mh.”] Na hali hiyo ya wasiwasi imekufanya uwe na mgandamizo wa damu, pia. Nawe umekuwa na kifafa. [“Hiyo ni kweli.”] Ndivyo ilivyo. Aisee, umekuwa aidha mhubiri, ama wewe ni mhubiri. [“Ni muhubiri.”] Sasa wewe ni mhubiri; nimekuona umesimama mimbarani. Basi, mwamini Mungu, ndipo huo wasiwasi utakuacha. Wahudumu wote huwa nao. Utapona. Rudi mimbarani mwako, na umtii Mungu na uwe mwaminifu kwa hilo Neno, Yesu Kristo.

¹⁹² Unaamini ugonjwa wako wa mgongo ulikuacha, ukiketi kwenye kiti kile? Unaamini jambo hilo? [Huyo dada anasema, “Naam.”—Mh.] Vema, bwana, basi endelea kusonga mbele, ukisema, “Asante, Bwana.”

¹⁹³ Njoo, bibi. U hali gani? Unaamini kwamba mimi ni mtumishi wake? [Dada anasema, “Hakika ninaamini.”—Mh.] Vema. Unaamini huo ugonjwa wa kina mama, ugonjwa wa wanawake, utakuacha? [“Amina.”] Unaamini? Basi endelea, useme, “Asante, Bwana.”

¹⁹⁴ Ugonjwa wa figo, ugonjwa wa mgongo, kwenye mgongo wako. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya, kutokana na hayo? Unaamini ya kwamba atakupa afya? Vema, chukua nini yako . . . ? . . .

195 Njoo, bibi. Mimi ni mgeni kwako. Kama nisingalisema jambo lo lote kwako, kamwe, ungeamini ya kwamba Uwepo wa Mungu upo hapa kuwaponya wagonjwa? [Yule dada anasema, “Hakika, naamini.”—Mh.] Ungeamini? Vema, kama unaamini, shida yako ya tumbo. . . Tayari nimekwambia, unaona. Ime—imekwisha. Nilikwambia, unaona. [“Bwana ashukuriwe! Loo, asante, Yesu.”]

196 U hali gani, bwana? Mungu huishi moyoni. Na moyo wako umekuwa ukitokea hapa muda kidogo uliopita, ni mgonjwa. Unaamini ya kwamba atauponya? Nenda zako na uamini jambo hilo. Mungu akubariki. Amini; atauponya.

197 Wewe una wasiwasi, umekufanya uwe na ugonjwa wa tumbo, vidonda vya tumbo. Vinakusumbua baada ya kula. Unaamini vyote vimeondoka sasa? Nenda ukajitafutie kitu cha kula.

198 Kwa namna fulani ni vigumu kwako kuamka, mgongo umekuwa ukikusumbua sana. [Huyo mgonjwa anasema, “Ndio, bwana.”—Mh.] Hautakusumbua tena, kama utaamini jambo hilo. Sivyo? [“Naam, bwana?”] Vema, nenda zako, na Bwana Yesu na akuponye kabisa.

199 Una wasiwasi wa nini? Nenda zako, useme, “Sitakuwa na wasiwasi tena,” nawe hutakuwa nao. Nenda na uamini. Vema, bwana.

200 Njoo, bibi. Sasa, yule mwanamke wa Kushi, mwanamke wa kizungu, kitu kama hicho kabisa vilikutana kwenye siku ile, Yesu. Wao walikuwa na ubaguzi kama waliokuwa nao Kusini, bali hatunao tena. Yesu aliwajulisha ya kwamba watu wote walikuwa watu wa Mungu. Hapakuwepo na tofauti, unaona, kama alikuwa Myahudi ama Msamaria.


201 Sasa kama Mungu hakusaidii, karibuni sana hiyo yabisi kavu itakulemaza. Bali unaamini Yeye atakusaidia, akupe afya? Kama tu vile yule mwanamke alivyofanya, nenda zako ukawaambie watu wako mambo makuu ambayo Mungu amekutendea. Vema.

Sasa, kuna daktari wa upasuaji aliye tayari kuchomoa kisu.

202 Hebu kidogo. Haikuwa ni mwanamke huyu. Sasa, hebu kidogo, kila mtu awe na kicho sasa. Ni—ni Shetani, alijaribu kufanya jambo fulani. Hili hapa. Kivimbe, kivimbe, ninyi nyote wawili. Sawa. Una kivimbe, yeye ana kivimbe, na huyu pepo anapiga makelele apate usaidizi kutoka kwa huyo mwingine. Bali Roho Mtakatifu anapiga makelele, pia. Utaamini nani, Yeye? Vema. Ondoka kwenye kitanda hicho cha wagonjwa, bibi. Simama utoke kwenye machela hayo. Ondoka humo, na uamini. Nenda zako, mwamini sasa. Amina.

203 Unaamini? Yote yanawezekana. Unaamini? Vipi ninyi kwa wasikilizaji? [Kusanyiko na hao ambao ndio kwanza waponywe wote wanashangilia—Mh.]

²⁰⁴ Hebu tusimame kwa miguu yetu sasa. Sasa hivi ndio wakati wa kufanya jambo hilo. Hebu kila mtu... Mungu akubariki. Hebu kila mtu asimame kwa miguu yake sasa hivi. Msifuni Mungu. Inueni mikono yenu.

²⁰⁵ Asante, Bwana Yesu! Tunakusifu kwa ukuu Wako, na kuponya Kwako wagonjwa. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] 

USHUHUDA BAHARINI SWA64-0307

(A Testimony On The Sea)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, Machi 7, 1964, katika Hekalu la Souls's Harbor, huko Dallas, Texas, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org